

SAUTI ISIYOJULIKANA

 Nilifurahi sana kuwa hapa asubuhi ya leo, nasi tunatumainia baraka nzuri za Bwana ziwe juu ya kila mmoja wenu. Wala sikujua kuwa ningekuwa hapa, kidogo linashangaza kwangu. Lakini waliuahirisha mkutano, kule Ujerumani, juma moja zaidi, kwa sababu ya jambo fulani lililotukia, ilibidi wautumie uwanja huo wa michezo. Kwa hivyo hatuendi hadi ju—juma moja kutoka Jumapili ijayo.

² Jumapili ijayo, tutakuwa... Jumamosi na Jumapili ijayo, kwenye viwanja vya kambi vya Methodisti huko Campbellsville, Kentucky, kwa ajili ya uamsho wa uponyaji. Jumamosi usiku itakuwa ni ibada ya uponyaji huko Campbellsville, viwanja vya kambi vya Methodisti. Jumapili ijayo alasiri, ninataka kuhubiri Ujumbe wa Injili, Bwana akipenda. Na kisha Jumapili usiku, tena, kutakuwa na ibada ya uponyaji kwa watu huko chini... Huko ni karibu na mji wangu wa nyumbani, ambako nilizaliwa na kukulia, au kuzaliwa. Nami nililelewa hapa Indiana. Kwa hiyo ninyi ambao mna marafiki ambao mmekuwa mkitaka kuja kwenye ibada ya uponyaji, vema, Bwana akipenda, tutakuwa huko Jumamosi ijayo alasiri, ama jioni, hasa. Nadhani utaanza kama saa moja na nusu. Mchungaji wetu mpendwa ataenda pamoja nasi, kufanya uimbaji na kadhalika.

³ Na kutakuwa na ibada maskanini, hapa, Jumapili ijayo asubuhi na Jumapili jioni. Na kutakuwa na m—mhudumu mzuri sana hapa kuwazungumzia, jambo la kushangaza. Kwa hiyo, nitaliacha tu hivyo, kwa sababu tunajaribu kupata mtu ambaye atakuwa ni mshangao kwenu kwa ajili ya Jumapili ijayo. Na kwa hiyo sasa, ninyi ambao hamwezi kuwa kule chini Campbellsville, kuwa pamoja nasi katika huo mkutano, mbona, njoni moja kwa moja kwenye hii maskani ndogo, na ibada zitaendelea kama kawaida, Jumapili ijayo asubuhi na Jumapili jioni.

⁴ Tungeondoka, ikitokea kuna mtu hapa kutoka karibu na Campbellsville, kwa kawaida sisi hujaribu kuondoka kwa ajili ya ibada, lakini wapo... tuna watu ambao kamwe hawawezi, kwenye wakati huo, kufika kwenye mikutano hiyo. Na tutakuwa na ibada haswa kwa ajili yao na hawa jamaa wadogo. Kwa hivyo, kila mtu amealikwa kwa moyo mkunjufu kwenye ibada hizi nzuri.

⁵ Kisha, imetokea tuna... Sasa kuzungumza tu juu ya wakati, jinsi unavyoongezeka kweli. Hebu wazieni. Nitaondoka hapa saa tano, asubuhi, kutoka Louisville. Na alasiri inayofuata, mara baada ya chakula cha mchana, ninahubiri huko Luxembourg, na Frankfurt, Ujerumani. Hebu wazieni tu, kuanzia saa tano hapa, kwenye... Ninaondoka Louisville saa tano, na alasiri inayofuata

ninahubiri huko Frankfurt, Ujerumani; kukiweko na tofauti ya saa tano, katika wakati, kuondolewa kwake, kutoka kwa huo wakati. Wazieni tu hilo! Jamani! Ni vigumu kuamini, sivyo? Upesi sana! Lakini ilitokea, kwa neema ya Mungu, kwamba tulipata usafiri mzuri wa moja kwa moja, PC-9 kutoka hapa hadi New York; na, kuanzia hapo na kuendelea, kwa Pan American. Inatupeleka moja kwa moja hadi Frankfurt.

⁶ Nasi tutakuwa huko si—siku kadhaa, halafu tutoke huko hadi Berlin. Na pamoja na—na Hal Herman maarufu, nitakuwa pamoja naye siku mbili usiku Berlin, Ujerumani. Yule mkurugenzi maarufu wa sinema aliyeongoka, wa Hollywood, naye aliongokea katika mojawapo ya hiyo mikutano huko nje. Naye ni Mjerumani, kwa kuzaliwa. Naye amerudi Ujerumani, akihubiri Injili chini ya hema kubwa huko Berlin. Na maelfu mengi wanatoka nyuma ya pazia la chuma. Ni . . .

⁷ Hakika ni jambo la kusikitisha. Asubuhi moja, nilikuwa nimeketi Zurich, Uswisi, na, basi, kulikuwa na watu wengi sana. Tulikuwa na watu mia moja na ishirini na sita elfu mkutanoni, kwa hivyo ilikuwa vigumu kutoka mahali hapo. Na kwa hivyo kila mtu, mnajua, jambo la kuhuzunisha, huku wakisihi waombewe, na kutaka kujua yale Bwana angewaambia.

⁸ Naye Bwana akaniambia, “Ondoka ushuke kuelekea ufuo wa bahari, ama ufuo wa ziwa.” Uswisi ni nchi ya kupendeza sana.

Nami nikasema, “Billy, tembea pamoja nami.”

⁹ Akasema, “Sasa, baba, unaelekea kujivuruga huko nje, na itakubidi kuwaita polisi wakutoe humo.”

¹⁰ Nami nikasema, “Vema, Bwana ananiambia nishuke kuelekea ufukoni.” Kwa hivyo nikashuka nikaenda huko, hakuna mtu. . . Wajerumani, na Waswisi, na Wabelgiji, na Ufaransa, na Waitaliano, mkutanoni. Hakuna mtu aliyenitambua, hata kidogo. Nilikuwa nikitembea moja kwa moja pale. Nami kidogo ninayo njia ya kujificha nisitambulikane, kidogo. Nina shaka kama ndugu yangu mwenyewe angenitambua kama wangekutana nami, mnaona. Hivyo . . . Naye alikuwa . . .

¹¹ Nilikuwa nikitembea moja kwa moja, nasi tukapanda pale na kuketi. Naye Billy akasema, “Mbona, unajua wananjua, baba.”

¹² Nikasema, “Vema,” nikasema, “wanaweza kukujua. Lakini,” nikasema, “Bwana aliniambia nije huku juu.”

¹³ Kasema, “Lakini Bwana anataka ufanye nini?” Ukosefu wa subira wa mtoto, mwajua.

Nikasema, “Atalishughulikia hilo.” Mnaona?

¹⁴ Kwa hiyo tukaanza kurudi nyuma, ubavuni mwa ufuo. Nikamwona mzee mmoja ameketi pale, akilia, akisoma, namna hiyo. Nikasema, “Yule pale. Yule ndiye.”

Akasema, “Hutapanda pale na kuzungumza na mtu yule?”

¹⁵ Nikasema, “Hapana, atakuja huku na kuzungumza nami.” Nikasema, “Yeye...” Nikasema, “Sasa yeye ametoka mbali sana.” Kisha nikasema, “Amekuja hapa; ni hali ya dharura. Angalia uone ikiwa mtu huyo hana kitu kwa ajili yangu. Na inahusu mkono wa mwanamke. Unaona?” Nikasema...

Kasema, “Unajuaje?”

¹⁶ Nikasema, “Ono limetokea hivi punde, na huyo ni mtu yule yule, huyo ni yeye anayeketi pale pale.” Na kwa hiyo nikasema, “Angalia tu upande huo mwingine sasa, upitie karibu naye.”

¹⁷ Tukaendelea mbele. Katika dakika chache, akasema, “Baba, mtu yule anatufuata.”

¹⁸ Nikasema, “Ninajua. Pia tutapiga kona; tutavuka daraja dogo, naye ataenda mbele yangu na kunipita pale pale darajani. Angalia kama hatafanya hivyo.”

Akasema, “Sawa.”

¹⁹ Kwa hiyo, tukaendelea mbele. Ndipo hapo akasimama, akapita mbele yangu, ndipo akanipita moja kwa moja kwenye daraja dogo. Akasema, “*Dugu Branham?*”

²⁰ Ndipo akatoa kwenye ninii yake ndogo... alikuwa na mfuko mdogo, kama kifurushi cha mwanamke, akatoa humo mkoba mdogo wa kitu fulani, pasipoti yake. Naye alitoka Urusi. Naye alikuwa na lesa mle ndani ambayo alitaka niombee, na kuipasua vipande sita, kwa ajili ya mwanamke pamoja na mkono wake mbaya sana ambao ulikuwa umejeruhiwa wala usingepona, nao unasinyaa. Naye alikuwa mama wa watoto watano. Vipande sita, mnaona, kamilifu tu.

²¹ Nami nikaangalia pasipoti yake. Alikuwa ametoka Urusi, huko nyuma ya pazia la chuma. Na kuwazia vile Bwana Yesu... Kuona maskini Mrusi huyo! Nikamwuliza walikuwa wangapi kule chini. Akasema, “Tuko mamia kadhaa tuliokwisha kupitia kwenye ngome na kuja kwenye mkutano wako.”

Nikasema, “Mlijuaje kuwa nilikuwa huku chini?”

Akasema, “Naam, tuliisikia kupitia redio ya Uswisi.”

Nami nikasema, “Je, mumewahi kusikia kuhusu ibada zangu huko juu?”

²² Akasema, “Wakati yule mvulana mdogo alipofufuliwa huko Ufini, hilo lilisambaa Urusi nzima.” Kote katika Urusi; mvulana yule mdogo alifufuka katika wafu. Kwa hiyo inaonyesha tu, Mungu anao watoto Wake kila mahali. Sivyote?

²³ Naye Hal Herman aliniambia, akasema, “Billy, tungekuwepo...” Unajua, ni karibu na ile ngome, huko Berlin. Akasema, “Kutakuwako, labda, na watu elfu tano, au watu elfu kumi, wamesimama. Unapofunga ibada, katika

dakika kumi (njia za chini ya ardhi) huwezi kumwona mtu.” Wanarudi nyuma ya pazia la chuma tena. Wanakuja kama fuko.

²⁴ Kwa hivyo inaonyesha tu kwamba licha ya makafiri wote, wote wasio haki, Unazi wote, Uhitla, na ufashisti, na ukomunisti, kamwe hautaishinda Nuru ya Injili. Bado iko katika mioyo ya watu. Nayo itaendelea mbele zaidi na zaidi, na zaidi na zaidi, na zaidi. Haitaisha.

²⁵ Kwa maana Yesu alisema, “Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu; wala malango ya kuzimu hayawezi kulishinda.”

²⁶ Je, hiyo si ni ajabu? Kujua ya kwamba sababu yenyewe ya wewe kuketi katika maskini jengo hili la kale lenye joto, asubuhi ya leo, huku feni zikipepea, ni kitu fulani ndani ya mtu kikiita, Nguvu zilizofichika ambazo ulimwengu hauna habari nazo. Ni wale tu ambao wamekuwa washiriki Wake, wanajua kwamba ni Nini.

²⁷ Je, zile spika ndogo zinafanya kazi huko juu sasa? Muda mfupi uliopita, ilikuwa ni vigumu kwangu kumsikia ndugu yangu mpendwa, kule nyuma, feni zinapepea, wa—wala nisingeweza kuelewa mengi aliyokuwa akisema.

²⁸ Vema, tuna furaha asubuhi ya leo kuwaona humu ndani, nje katika siku hii yenye joto. Msisahau ibada ya Jumatano usiku maskanini. Na ninadhani mtamsikia Ndugu Neville wakati uo huo, Jumamosi ijayo asubuhi, halafu huenda ikawa ata—ataendelea moja kwa moja kutoka pale, ashuke hadi Campbellsville basi, au jioni hiyo, hasa, kwa ajili ya ibada.

²⁹ Nami nina furaha kumwona mtoto Edith, na familia ya Wright tena asubuhi ya leo, Dada Lawton, wengi wenu hapa. Nami ningependa kumsikia Dada Angie na hao wengine wakiimba, “Humwongoza tai katika hewa isiyu na njia,” chochote kile, tulipokuwa tukiingia. Nilikuwa nikiufurahia.

³⁰ Nilikuwa nikijaribu kupeana mkono na Ndugu Fleeman, kule nyuma, na kuzungumza naye kwa muda kidogo. Na hivyo ndivyo. . . Sikuelewa ni nini hasa. Hebu tuone. . . ? . . . Mtu fulani hapa anataka. . . Ni maombi kwa ajili ya kiungo, mtu.

³¹ Vema, Jumapili iliyopita usiku tulikuwa na mkutano mzuri sana huko kwenye Kanisa La Mlango Wazi, Bwana akitenda mwujiza mkubwa huko. Na karibu imejaza nyumba yao na watu kabisa juma hi—hili. Kwa hivyo umekuwa ni wakati mzuri. Loo, hali ya joto sana. Lakini, hata hivyo, Mungu na ashukuriwe, tunaweza kuwa hapa nyumbani mwa Bwana, asubuhi ya leo, na tayari kumtumikia Bwana.

Twaweza kuomba?

³² Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru sasa hivi, katika Jina la Yesu, Mwanao mpendwa, kwa yote aliyotufanyia. Na kutusamehe dhambi zetu, na kutualika katika ushirika huu mzuri sana na wa ajabu wa mateso Yake, na ushirika huu wa

utukufu Wake uliofuata ufufuo, ili kujua hili dhahiri, kwamba Yesu alifufuka katika wafu na yuko hai miongoni mwetu leo. Jinsi tunavyompenda kwa yale aliyofanya! Kumwona, jinsi anavyowaponya wagonjwa, alivyomfanya msichana yule mdogo, kipofu (akisoma Breli), hivi majuzi usiku, macho yake yakafunguka, na kutembea humu jengoni, akiwathibitishia watu ya kwamba Yeye amefufuka katika wafu.

³³ Na sasa tunakuomba, loo, Mungu mkuu aliyefufuka, Mungu wa miungu yote, Mamlaka ya Upeo juu ya kila kitu kilichoko mbinguni na duniani, Mtawala na Mwenye Kubuni. Tunaomba kwamba Utu Wako mkuu utatubariki leo, na Ukuu Wako uingie katika kila moyo, asubuhi ya leo, Baba, na kuchukua mamlaka juu ya wote. Tunaomba kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

³⁴ Kwenye Kitabu cha Wakorintho wa Kwanza, kwa njia tu ya somo, kama tungeliita hivyo, kwa dakika chache, tungependa kusoma kifungu kimoja au viwili hapa, ili kutupa msingi na ushuhuda mdogo ambao nataka kuwaambia kabla hatujaanza kuongea.

³⁵ Nina muhtasari kidogo ulioandikwa hapa chini, wa mambo mbalimbali ninayotaka kuwaambia kuhusu ibada, pamoja na jambo lililotokea hivi majuzi. Kwa hiyo, sitaisahau, natumaini.

³⁶ Sasa, katika Wakorintho wa Kwanza. Neno la Mungu daima lina utangulizi. Ndilo la kwanza. Shika Neno Lake. Na sasa katika mlango wa 14, na kuanzia kifungu cha 6, nasoma hili.

Ila sasa, ndugu, nikija kwenu na kusema kwa lugha, i—itawafaidia nini, isipokuwa ninyi... nasema nanyi kwa njia ya ufunuo, au kwa njia ya elimu, au kwa njia ya hotuba, au kwa njia ya fundisho?

Hata kila kitu kisicho na uhai kikitoa sauti, ikiwa ni filimbi... kinubi, au kisipotoa sauti iliyo na tofauti, itatambulikanaje kama ni filimbi au kinubi?

Maana baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, ni nani atakayejiweka tayari kwa...vita? (Paulo akizungumza.)

³⁷ Na halafu katika Zaburi, Zaburi ya kwanza, tunasoma hili. “Heri mtu yule ambaye Mungu hatamhesabia udhalimu, au, dhambi.” Na mtu mwenye heri ni mtu tofauti. Daudi akinena, akisema jinsi vile alivyobarikiwa, kwamba, “Mtu mwenye heri, alikuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji,” katika Zaburi 1, “na jinsi ambavyo angezaa matunda yake kwa majira yake. Mtu asiye haki hangekuwa hivyo, lakini ange—angeangamia,” na kadhalika. Lakini, m—mtu mwenye heri alikuwa ni mtu wa Mungu.

³⁸ Na sasa nataka, kwa kuwa hakuna wengi sana hapa leo, nami natumaini si joto sana kwenu kuketi hapo, kwa dakika

chache, ama angalau dakika arobaini na tano. Ningependa tu kuzungumza nanyi, moyo kwa moyo, leo.

³⁹ Kwenye maskani, sipati nafasi ya kufanya hivi mara nyingi sana, ama huko nje mikutanoni, kufundisha mafundisho, au kusema mambo ninayotaka kusema. Lakini, huko nje, sikuzote ni juu ya masomo ya uponyaji wa Kiungu. Na huko nje katika makanisa mengine, ambapo tofauti zao huchanganyikana, na madhehebu fulani yanayofundisha theolojia mbalimbali, vema, basi, si—siwezi kulisema, kwa sababu linaumiza hisia, na kadhalika. Hata, wakati mwingine, Neno likihubiriwa, rahisi na dhahiri, linaumiza hisia. Basi jambo bora zaidi la kufanya ni kukaa tu kwenye kanuni za kimsingi za—za Yesu Kristo tunapokuwa huko nje, na kifo Chake, kuzikwa, kufufuka, na ngu—nguvu Zake na upendo kwa watu. Na hivyo halileti mchafuko.

⁴⁰ Kwa sababu, sininii. . . Kwangu mimi, haijalishi watu ni wa kanisa gani. Jambo muhimu ni kama wao ni Wakristo. Kama wewe ni Mkatoliki, kama wewe ni Mprotestanti, kama wewe ni Mmethodisti, Mbaptisti, ama chochote unachoweza kuwa; mradi wewe ni Mkristo, hilo ndilo jambo kuu. Kristo haangalii kanisa lako unaloshiriki. Kwa sababu, yote yataangamia na kuondoka siku moja, na kuvunjika, wala hayatakumbukwa tena. Lakini ka—kanuni ya Ukristo ni hali za moyo zinavyohusiana na Mungu. Na hilo ndilo jambo ambalo tunapenda kuzingatia; ni kumjua ndugu, si kwa kanisa analoshiriki, ama jinsi anavyovaa nguo zake, bali vile alivyo moyoni mwake.

⁴¹ Sasa, somo langu asubuhi ya leo, bila shaka, ni: *Sauti Isiyojulikana*.

⁴² Sasa kuna vitu vingi ambavyo hutoa sauti. Na kuna sauti nyingi zisizojulikana siku hizi. Kuna mashaka kila upande. Kila mahali unapoangalia, katika mambo ya kitaifa, ni—ni mashaka.

⁴³ Mikutano ya wale viongozi wanne, ni, wanakutana. Wanaandika maazimio, lakini kuna mashaka kama huo upande mwingine utatimiza ahadi ya—yao, au hautatimiza. Haijulikani kama mvua itanyesha kesho, au ikiwa kutakuwa na hali nzuri ya hewa. Kuna mashaka katika kila kitu unachoangalia, ila kitu kimoja, hicho ni katika Kristo. Mnaona? Hilo ni jambo moja ambalo unaweza kuwa na uhakika, ambalo ni yakini.

⁴⁴ Na kuna jambo lingine ambalo ni hakika kabisa kwa kila mtu hapa ndani. Ninataka kuwaachia wazo hilo, kwanza kabisa. Haijulikani kama utaishi upate kutoka katika kanisa hili au la. Haijulikani kama utawahi kurudi tena au hutarudi. Haijulikani kama utaona mwaka mwingine. Lakini kuna jambo moja ambalo bila shaka ni la hakika; hilo ni mauti, na Hukumu baadaye. Una hakika kukabiliana nayo kadiri Mungu alivyo Mbinguni.

45 Unaweza kufanya miadi na mkeo, na kusema, “Mpenzi, nitakupeleka mahali fulani.” Jambo fulani linaweza kutokea usiweze kufanya hivyo. Huenda usiweze kutimiza miadi hiyo.

46 Unaweza kumwambia rafiki yako msiri kabisa, “Ndugu, nitakutana nawe. Nitafanya jambo fulani. Nitakuruhusu upate pesa, au nitakupa gari langu.” Kila aina ya...kutokuwa na uhakika na hilo.

47 Lakini kuna jambo moja ambalo ni hakika, hilo ni, “Utakufa, na, baada ya hapo, utakabiliana na Hukumu.” Kwa hivyo zingatia hilo niani wakati tukizungumza juu ya kutokuwa na uhakika.

48 Sasa kuna watu wanaofikiria kwamba, “Maadamu tunaenda kanisani, maadamu sisi ni wa kanisa, maadamu tunasikia mahubiri mazuri mara kwa mara, na kadhalika, ya kwamba ni sawa.”

49 Sasa, kwa kuwa kuna joto na kadhalika, na ninatokwa na jasho hivyo, na chini ya feni hii na kadhalika, kwa kawaida hunifanya nipwelewe na sauti, ninataka tu kuzungumza nanyi leo, nikiweza, kuwafundisha, mambo fulani ambayo najua mnapaswa kuyajua. Na hilo ni jambo litakalokuboresha zaidi, ambalo litakusaidia safarini.

50 Natumai kwamba Mungu atanisaidia leo kuwapasha jambo fulani, litakalokufanya utambue kile unachopaswa kuwa na kile inakubidi kuwa, na, kwa kukwambia, pia kutanifanya nitambue, kwamba sina budi kuwa mtu bora kuliko vile nilivyo na vile nimekuwa. Na kila siku, hebu niinuke juu kidogo tu, karibu zaidi na Kristo.

51 Hilo ndilo lililotuleta hapa asubuhi ya leo, katika unyofu na uadilifu wa mioyo yetu, ninaamini tusingekuja kanisani, kuna joto leo, ambapo inatubidi kuketi hapa na kuteseka chini ya hili joto, kuwa tu tukija kanisani kwa furaha ya kuja, ninaamini kuna jambo fulani unalolijia, yaani, kwa ajili ya Kristo.

52 Kamwe huji kunisikia mimi. Ingawa ninaweza kufanya vizuri sana niwezavyo, lakini sijawahi kumvuta mtu yeyote kwa Mungu. Hakuna awezaye kuvuta ila Kristo.

53 Unakuja kusikiliza uimbaji, labda. Uimbaji ni mzuri sana. Tunapenda aina hiyo ya uimbaji. Lakini uimbaji hauwavuti watu kwa Kristo. Ni—ni Roho Mtakatifu anayewavuta watu kwa Kristo. Mnaona?

54 Kuhubiri hakuvuti, ingawa tunajaribu vizuri zaidi tuwezavyo. Mimi pamoja na mchungaji, tunafanya vizuri sana tuwezavyo ku—kuwavuta watu kwa Kristo, au kuihubiri Injili, bali ni Roho Mtakatifu Ndiye hana budi kuuvuta moyo wako na kukupa hiyo sauti inayojulikana. Tunaweza kuhubiri Injili, ya kile tunachofikiri ni kweli, lakini Roho Mtakatifu hana

budi kutoa sauti inayorudisha mwangwi moyoni mwako. Na kuna sauti inayojulikana.

55 “Ipo njia, pia, ione kanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia za mauti.”

56 Ni nje kidogo ya somo, lakini nataka kuzingatia hilo kidogo tu, kuhusu m—mtu fulani ambaye ninaweza tu kumwazia niani mwangu, mtu wa kubuni, na kumwita Bibi John Doe. Huyu Bibi John Doe, alipolelewa kanisani, alikuwa mwanamke mzuri. Alimpenda Mungu. Loo, alienda kanisani na mama yake. Alifundishwa ku—kutenda yaliyo mema.

57 Sasa, Mungu na atupe wengine zaidi wa wale akina mama wa mtindo wa kale watakaowafundisha wasichana na wavulana wao jinsi ya kutenda mema, kujua mema na mabaya! Hilo ndilo tunalohitaji leo. Tuna mifano mingine mingi sana mbele ya vijana wetu, kama vile, kuvuta sigara, kunywa pombe, karamu za pombe, na kadhalika, ambayo haipaswi kuwa, na inapitia kwa akina mama, wanaojiita hivyo.

58 Sasa angalieni. Ndani ya mwi—mwili wa mwanadamu, maumbile yetu, mwili wetu wa kawaida tunamoishi hapa, haujaumbwa upate kutenda dhambi. Umeumbwa kutenda haki. Umeumbwa kumtumikia Mungu.

59 Mungu kamwe hakukuumba kufanya kazi tu, na kuja nyumbani na kuwapenda watoto wako. Hayo yote ni mazuri kutosha. Mungu alikuumba upate kufanya kazi. Mungu alikuumba kuja nyumbani, uwapende watoto wako, umpende mkeo, naye mke awe mwaminifu na kumpenda mumewe; watoto wawapende baba na mama yao. Hayo yote ni mazuri. Lakini Mungu alikuumba . . .

60 Hiyo ni misingi tu kwa ajili ya kitu ambacho Mungu alikuumba upate kufanya. Mungu alikuumba kuwa mwabudu, mwabudu Wake. Utaabudu kitu bila kujali ni nini. Utamwabudu mkeo. Utawaabudu watoto wako. Utaabudu chochote; gari lako, ninii yako . . . Utaabudu anasa zako. Utaabudu kitu fulani kwa sababu kuabudu kuko ndani ya wanadamu. Sasa tunataka kujua kile tunachoabudu.

61 Yesu akamwambia yule mwanamke kisimani, akasema, “Mnaabudu, msichokijua. Sisi Wayahudi, tunaabudu . . . Tunajua kwamba tunamwabudu Mungu, kwa sababu wokovu ni wa Myahudi.”

62 Sasa, na ndipo huyo mwanamke akaanza kumwelezea jinsi yeye . . . “Mmoja alisema, ‘Mlimani,’ mwingine akasema, ‘Yerusalemu.’”

63 Yeye akasema, “Saa yaja, na sasa ipo, wakati Baba atakapowatafuta waabuduo watakaomwabudu katika Roho na katika Kweli. Kwa maana Mungu ni Roho, nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika Roho na Kweli.”

⁶⁴ Kama nilivyokuwa nikisema, siku chache zilizopita, ama hapa au mahali fulani, nikizungumza kuhusu kigundua uongo. Sasa angalieni kwa makini sasa. Nataka msikilize kwa makini. Weka kigundua uongo juu yako, kisha ujaribu kuiga ninii... ukweli huo, na ujaribu kusema kuwa ni ukweli, lakini chini ndani yako, katika dhamira yako ya ndani, kuna mahali panapoitwa nafsi. Nayo nia hii ya kiakili haidhibiti mtetemo huo wa huo mfumo. Nia ni mkurugenzi tu. Itakuelekeza, wala haina uwezo kabisa wa kukuleta kwa Mungu; nia yako. Huwezi kumjua Mungu kwa nia yako, kiakili. Ni mojawapo ya rasilimali, au njia ambazo zingeongoza kwake, lakini nafsi yako ndiyo inayokutawala. Wewe u kile ulicho, kwa nafsi yako.

⁶⁵ Yesu alimwambia yule Farisayo, kasema, “Mbona, enyi wanafiki. Mwawezaje kusema mambo mazuri?”

Wakati, walipokuwa wakimwita, “Mwalimu mwema,” na kadhalika.

⁶⁶ Kasema, “Kinywa hunena yaujazao moyo. Na moyoni mwako unanichukia Mimi. Na midomoni mwenu mnaniita, ‘Mwalimu mwema.’” Akasema, “Enyi wanafiki!”

⁶⁷ Unaona, nafsi yako inawaza jambo moja, nawe unazungumza kwa midomo yako jambo lingine! Ni kisa cha jinsi gani! Ni jambo baya jinsi gani! Mnafiki ni kitu kidanganyifu jinsi gani! Kwa maana, kutoka niani mwao wanasema jambo moja, wakati nafsi yao inasema jambo lingine.

⁶⁸ Sasa, kigundua uongo hakitafanya kazi niani mwako. Kitafanya kazi nafsini mwako. Hakitafanya kazi kwenye akili zako. Kuna baadhi ya watu wanaoweza kuiga ukweli. Wanaiga. Hata hivyo, ukiwa ni uongo, nao wanaweza kuuiga mpaka wanaweza kudanganya kama kitu chochote kile.

⁶⁹ Na Shetani ndiye bora zaidi wa huo aliyepo, kwa maana amemtanganya Hawa kwa njia hiyo, akisema mambo hayo hayo. Basi uongo mkubwa zaidi, uliowahi kusemwa, ulikuwa na ukweli mwingi ndani yake.

⁷⁰ Sasa, mtu huyu, vipi kama ungeweza kuifanya nafsi hii ya ndani, kuwa katika upatanifu mkamilifu na Mungu, hata nafsi yako na Mungu viwe kitu kimoja, pamoja, basi ungeweza kuomba utakalo nawe utapewa.

⁷¹ Watu wengi hunijia, mara nyingi kwenye mstari wa maombi, na kusimama hapo na kusema, “Loo, Ndugu Branham, nina imani tele. Nina imani kama ya kuhamisha milima.” Na, hata hivyo, hawana imani yoyote. Karibu hawana imani ya kutosha kufika jukwaani. Lakini wanatambua jambo moja, kwamba wanaamini. Wanaamini kiakili kwa nia zao. Wala nia zao kamwe hazitawaleta kwa Mungu. Nia yako ni hoja. Naye Mungu hana hoja.

⁷² Kama unaweza kulihoji kabisa, nia yako itakwambia, “Sasa angalia hapa, daktari anasema siwezi kupona huo. Haiwezekani.”

⁷³ Sasa, daktari, kwa akili zake, na bongo lake, pamoja na maarifa yake ya sayansi ya matibabu, amekwambia yaliyo bora zaidi akili zake zinayoweza kufikia. Nawe unayaweka niani mwako, na ukitumia kitu kile kile ambacho daktari amekwambia, wewe... Mungu hawezi kamwe kugusa mstari huo, maadamu unatoa hoja. Lakini hebu tuweke kando hoja. Mungu hakutuumba tuishi kwa akili zetu. Tunaishi kwa Roho Mtakatifu aliye ndani ya nafsi zetu, anayesema “la” kwa hoja yoyote iliyo kinyume na Neno la Mungu.

⁷⁴ Neno la Mungu linaposema ndivyo ilivyo, hakuna kitu ulimwenguni kinachosimama katika njia Yake. Ndipo unapofanya hivyo, unashuka chini upande wa kuume wa Mungu. Unashuka mpaka unaweza kuomba unachotaka, nawe utapewa, kwa sababu hakuna kitu kilicho hapo katikati. Hakuna hoja. Tuachane na hoja hizo. Zinakuzuia. Ondolea mbali nia yako. Wala usiseme hoja yako, unachokiona, unachowazia. Sema anachosema Mungu kuwa ni Kweli. Na hicho kinaweza tu kutoka ndani, kutoka moyoni, sio kutoka akilini.

⁷⁵ Hapo ndipo watu wengi sana, siku hizi, watakapopata masikitiko sana katika Siku ya Hukumu. Kujua kwamba wameishi kanisani, kujua kwamba wamefanya matendo mema, kujua kwamba wamemtendea jirani yao haki, kujua kwamba wamekuwa waaminifu kwa watu, waaminifu kwa kanisa; na niani mwao waliamini kwamba, Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, kisha wahukumiwe kwenye Siku ya Hukumu.

⁷⁶ Yesu alisema, “Wengi wameitwa na wachache wamechaguliwa. Mlango ni mwembamba na njia imesonga iendayo Uzimani, nao watakaoina ni wachache.”

⁷⁷ Sasa kwenu ninyi watu hapa asubuhi ya leo, ni—ninawatakeni mketi kitako na kulizingatia hili. Mna umri wa kutosha sasa. Mmesikia Injili ya kutosha ikihubiriwa mpaka mnapaswa kuweza ku—kuachana na maziwa, na kuja kwenye mlo mgumu kweli wa Injili; mfikie mahali ambapo wanaume na wanawake wanapaswa kusimama. Paulo alisema, “Mnapopaswa kuwa waalimu, mbona, inawabidi kufundishwa, bado.”

⁷⁸ Sasa katika nafsi, aishipo mtu, wewe ni kile ulicho nafsini mwako. Si niani mwako, si katika hoja zako, si kwa sababu unasema, “Nitakuwa na msimamo mzuri zaidi. Ninaweza kushirikiana na watu bora zaidi kama nitakuwa Mkristo.” Hiyo ni hoja. Unaona? Hupaswi kufanya hivyo. Usifanye hivyo. Acha iwe ni ya kutokana na ujuzi mpya, Kuzaliwa upya; jambo ambalo limetokea sio akilini, bali nafsini, ambalo limeondolea mbali hoja zote, nawe unakuwa kiumbe kipya. Ndipo wewe uko katika Kristo Yesu.

⁷⁹ Bibi John Doe, alikuwa mwanamke mzuri, tujuavyo sisi. Aliolewa na Bw. Doe. Alikuwa mwanamume mzuri Mkristo. Kwenye umri wa kama, loo, miaka thelathini, ama kitu kama hicho, Bibi Doe alikuwa mwanamke wa kuvutia. Anaenda na kuanza kushirikiana na majirani. Anatoka anaenda miongoni mwa umati wa kilimwengu. Sasa, angalia, anatoka nje miongoni mwa huo umati. Anaanza kushirikiana na hao watu wengine; sio watu wabaya; watu wema, watu wa kidini labda katika ujirani wake. Anaanza kushirikiana na watu hao. Na huku akishirikiana na watu hao... Anajua kuwa yeye ni mwanamke mzuri.

⁸⁰ Ndipo muda si muda mwajua, kitu fulani kinamshika. Anavutiwa na mwanaume mwingine. Mbona, yeye ni mwanaume wa kuvutia sana. Anavutia zaidi kuliko mumewe. Ndipo kitu kinatokea ndani yake, kwamba anahisi anampenda mtu huyu.

⁸¹ Sasa sikilizeni. Ndani kabisa ya nafsi yake, Neno la Mungu linaanza kuchemka, na kusema, “Umekosea. Nadhiri yako ni kwamba ‘utashikana na mwanaume huyu mpaka kifo kitakapowatenganisha,’ hata awe na sura gani.”

⁸² Ni mwanamke au mwanamume anayevutia zaidi jinsi gani, na inafanya kazi kwa pande zote mbili. Umeweka nadhiri kwa mtu huyu hadi kufa, unajitenga. Lakini utaendea mambo ya kiakili. Utawazia, “Huyu hapa Bibi Jones. Anacheza piano. Yeye ni mwanamke mzuri. Mbona, amefanya *hivi*,” na kutoa hoja. Utaona hao wanawake wengine wakianza kuvalia kizinifu, hata wanavaa maskini nguo hizo fupi wanazovaa msimu wa kiangazi huku, zaidi sana, katika majira ya baridi kali kama wangeweza. Kwa urahisi ni wachafu tu! Nawe utatoka nje.

⁸³ Sasa, kina mama, nataka mnisamehe. Sitaki kuumiza hisia zenu. Siko hapa kuumiza hisia zenu. Mungu anajua sivyo. Lakini niko hapa kama mhubiri wa Injili, kukujulisheni ukweli, ndipo mfanye nao chochote mtakacho. Basi unapoanza kufanya mambo hayo, utanza kutoa hoja, “Ikiwa mwanamke huyu anaweza kufanya hivyo! Ana sifa nzuri. Anaenda kanisani. Ana cheo katika jamii. Kwa nini nisifanye hivyo?” Hiyo ni hoja, wakati nafsi yako inakwambia ni kosa. Mungu aliwafunika wanawake, na mwanaume, katika bustani ya Edeni; kamwe hakuwavua nguo. Mnaona? Lakini ni kuhoji. Utatoa hoja, “Wengine wao wanafanya hivyo.”

⁸⁴ Wasichana wadogo, ninyi—ninyi izingatieni asubuhi ya leo Injili. Injili ilisema, “Wanawake na wajivike mavazi ya kujisitiri,” sio machafu, “mavazi ya kujisitiri.” Na inakuwa... Ni aibu.

⁸⁵ Mnajua kile kingetukia katika Zurich, Uswisi, kama mwanamke akishuka kuja mtaani akiwa amevaa kama wanawake hawa wanavyofanya huku Marekani?

Wangemtupa gerezani papo hapo na -tangaza... kukutangaza mwendawazimu. Hakika.

⁸⁶ Nilipokwenda Urumi, Italia, nikakwea yale maeneo ya kuwazikia watakatifu, hata walikuwa na ubao langoni, kwenye makaburi ya Mtakatifu Angelo, mapango ya kuzikia, na kusema, “Wanawake wa Marekani, tafadhali vaeni nguo kabla ya kuingia mahali hapa, ili kuwaheshimu wafu.” Na mahali pakaidi, pa aibu, palipoharibika, duni kama Italia, na inawabidi kunena maneno kama hayo. Nao wahubiri wetu ndio waliosababisha hayo, kutoka jukwaani, kwa kutosema Ukweli. Amina. Hiyo ni kweli.

⁸⁷ Angalieni, huyo mwanamke anaendelea. Anafikiri yuko sawa. Baada ya kitambo kidogo, anamwacha mumewe. Anaondoka na kuolewa na mwuzaji huyu msafiri, kwa sababu yeye ana sura nzuri, jamaa mkubwa. Ndipo baada ya muda mfupi anakuta kwamba yeye si mtu kama mumewe alivyokuwa. Mnaona, yeye si mkarimu, kama mumewe alivyokuwa.

⁸⁸ Na baada ya muda kidogo, basi, anawazia, “Loo, vema, nimefanya hivyo, nitapendana na mtu mwingine.” Anaendelea. Anasafiri. Anaenda kanisani, sikuzote. Mchungaji hajawahi kuliondoa jina lake kwenye kitabu. Anaenda moja kwa moja kanisani. Anaishi kama vile tu anavyotaka kuishi.

⁸⁹ Basi muda si muda mwajua, loo, nawe unasema, “Sasa angalia, Bibi Doe, unamwamini Yesu Kristo?”

⁹⁰ “Kwa moyo wangu wote ninamwamini.” Lakini matendo yake, matunda yake, yanathibitisha kwamba hamwamini. Usisikilize sauti isiyojulikana. Acha itoe sauti kutoka kwa Injili hapa. Inathibitisha kuwa hamwamini. Kwa maana, hangekuwa akifanya mambo hayo. Asingekuwa akitenda hivyo. Angekuwa na mawazo tofauti. Angetawaliwa na kitu tofauti; nafsi yake.

⁹¹ Mara ya kwanza alipomhuzunisha, kule nyuma, alipoanza kutoka nje, akimkimbia mumewe. Hii hapa akili yake hapa; hii *hapa* nafsi yake hapa. Kuna mstari unaotenganisha hapo, ambao kama ikiuvuka kamwe, haitarudi tena. Haitarudi kamwe. Wazia hilo. Naye anaendelea.

⁹² Ndipo baada ya kitambo kidogo, anapotenda dhambi dhidi ya kitu hiki kilicho ndani yake, kinachonena juu ya Neno la Mungu, muda si muda mwajua, atahusika na haya mambo ya kiakili, aachane na nafsi. Biblia ilisema, “Nafsi itendayo dhambi, nafsi hiyo itakufa.” *Kufa* maana yake ni “kutengana.”

⁹³ Halafu, hiyo nafsi, dhamiri ambayo wakati mmoja inakuhukumu, haipo tena, na umeingia kwenye mambo ya kiakili kabisa. Unaenda unajiunga na maskini kanisa baridi la kale, la kawaida, ambalo haliadini katika mambo hayo. Anaendelea na kuingia kwenye anasa, na, muda si muda wajua, ile nafsi inayokuhukumu mara ya kwanza uliposema uongo, mara ya kwanza ulipovaa nguo hizo fupi, mara ya kwanza

ulipofanya uovu, itakuwa imekufa sana kwako, hutaihisi tena. Utaendelea mbele zaidi na zaidi. Na baada ya kitambo kidogo mauti itakupata.

⁹⁴ Unaishi huko nje. Mchungaji wako atakuja na kusema, “Mambo yote ni sawa, dada yangu. Uko tayari kwenda sasa. Kila kitu ni shwari.” Ataamini vivyo hivyo. Ndipo muda si muda mwajua, inapofikia . . .

⁹⁵ Kwa nini? Pamoja na uwezo wote wa kutoa hoja alio nao! Ameenda kanisani. Ametoa misaada. Amefanya kila kitu kilicho sahihi, ndivyo anavyowazia, kila kitu kilicho sahihi niani mwake. Amefuata maagizo ya nia yake. “Najua napaswa kwenda kanisani. Najua ninapaswa kuwapenda watu. Najua napaswa kumtendea jirani yangu haki. Najua napaswa kufanya *hivi na vile*.” Lakini, bado, ni kitu gani? Amemhuzunisha Jamaa *huyu*.

⁹⁶ Halafu basi, katika saa ya kufa kwake, anapokuwa tayari kufa, amelala kitandani. Na, mara ghafla, anaamka na kupiga mayowe, “Loo, Mungu wangu! Nimepotea.”

⁹⁷ Mchungaji atasema, “Mpe kituliza akili. Ana mpagao.” Naye atamdunga kituliza akili. Naye atajaribu kuongea. Hawezi kuongea. Atanong’oneza.

⁹⁸ Ni kitu gani? Nafsi yake imemfikia, kabla hajafa. Si wanawake tu; wanaume, pia, walioukataa upendo wa Yesu Kristo, ambao wamemkataa, wakamdhihaki. Itakupata siku moja, hakika kama ninavyosimama hapa asubuhi ya leo. Umeihuzunisha sana, hata huwezi kuihisi tena. Lakini itakupata wakati mmoja, tena. Yote yatakurudia, yale mambo machafu, yale mambo mabaya, umbeya, uropokaji, masengenyo, ubinafsi, na mambo ambayo umefanya. Hayo yote yatakurudia, siku moja, ukiwa umelala kwenye kitanda cha mauti.

⁹⁹ Jinsi sindano ya kutuliza akili katika siku hizi za mwisho imeyakomesha maungamo ya kitanda cha mauti ya maelfu ya watu! “Mdunge sindano. Mtie ganzi.” Anajaribu kunena.

¹⁰⁰ Ni kitu gani? Nafsi yake imemfikia hapa. Nafsi hiyo na roho ni kitu hiki hapa, ambacho mwenye akili anajaribu kukishinda. Kiko tu akilini. Mambo ya kiakili, yale uliyoishia, yataangamia. Lakini nafsi hiyo uliyoihuzunisha kwa mambo yako ya kiakili, itakurudia kote katika Umilele. Amina.

¹⁰¹ Usisikilize sauti isiyojulikana. Amini Injili, katika utimilifu wake. Naam, bwana. Loo, wasema, “Nilienda kanisani. Nilifanya yaliyo mema. Nilitoa zaka zangu.” Mambo hayo ni sawa, lakini hayo ni mambo ya akilini.

¹⁰² Basi angalieni, wakati wanapojaribu kunyamazisha, kwa sindano hiyo ya kutuliza akili mikononi mwao, kuwatia ganzi ili wasijue lolote, nao wanajaribu kuzungumza. Nafsi

yao imewafikia. Wanatambua kwamba hoja zao, nia zao, zinaangamia pamoja na ubongo wao.

¹⁰³ “Ati zinaangamia pamoja na ubongo wao, nia?” Naam, bwana. Naam, bwana. Nia yako itaangamia pamoja na kifo chako.

¹⁰⁴ Nitawathibitishia. Kigundua uongo hakipimi nia yako; kinapima nafsi yako. Mtetemo wa mishipa yako haipitii kwenye nia yako; inapitia nafsini mwako. Amina.

¹⁰⁵ Kwa hivyo, akili zako zitakufa wakati ubongo wako unapokoma kufanya kazi. Wakati damu inapokosa kupitia ubongoni mwako, nayo mishipa inakoma, basi nia yako inaondoka nayo nafsi yako inakufikia.

¹⁰⁶ Basi wakati nafsi ya mwanamke huyu inapomfikia, naye anasema, “Mungu wangu, nimepotea.”

¹⁰⁷ Na wanafikiri ni, loo, ni mpagao. Wanamdunga sindano ya kutuliza akili, sindano kwake, naye anaanza kufa ganzi. Hawezi kuongea tena. Anajaribu. Anajigaragaza. Ana maumivu makali. Naye daktari anasema, “Mdunge nyingine; kumtia ganzi,” mpaka malaika wa mauti atakapoiondoa ghafla roho yake kutoka kwake.

¹⁰⁸ Lakini, sindano hiyo inaweza kuutia mwili wake ganzi, inaweza kutia ganzi nia yake, lakini hiyo haiwezi kuitia ganzi nafsi hiyo inayojua kwamba ilitenda dhambi mbele za Mungu. Itamsumbua katika nyakati zisizo na kikomo, na katika Umilele. Nafsi hiyo bado itasumbua tena na tena na tena, kadiri nyakati zinavyoendelea.

¹⁰⁹ Ulitoka wapi? Unaenda wapi? Ulitoka katika Umilele. Ukaingia kwenye sehemu ndogo inayoitwa wakati. Unatoka kwenye wakati na kuingia katika Umilele. Basi vile ulivyo nafsini mwako, unapotoka, ndivyo utakavyokuwa. Loo, jamani. Vema.

¹¹⁰ Hiyo ni bora kidogo sasa? Ninapata tu... Ninaona, inatoa sauti kubwa kidogo kwake. Vema. Wa—wakati ninii... [Mfumo wa PA unatoa mwangwi—Mh.] Naamini ananinii... Ni kwa Ndugu Neville. Kidogo ninahubiri kwa nguvu.

Vema, kuingia katika Umilele, haya basi.

¹¹¹ Mchungaji fulani atamjia huyo mwanamke, aseme, “Vema, dada yetu mpendwa, alikuwa mshiriki mwaminifu sana katika kanisa letu. Alikuwa kila siku ya sabato. Aliwasaidia maskini. Aliwasaidia wahitaji. Alifanya mambo haya yote. Leo yuko Utukufuni.”

¹¹² Lakini, laiti ukweli ungejulikana, huko mahali pa mateso panapoitwa kuzimu, nafsi hiyo iliyojitenga naye hapa duniani, ambapo alisikiliza sauti isiyojulikana. Naye akaenda zake katika Umilele bila ya kumjua Mungu, bila kumjua Kristo kama

Kuzaliwa upya. Aliliamini moyoni mwake. Aliliamini niani mwake. Alifikiri alikuwa sahihi, lakini alikuwa makosani.

Ni nafsi yako, inayofanya hivyo. Ee Mungu, uturehemu!

¹¹³ Sikiliza sauti iliyo dhahiri. Injili haina sauti isiyojulikana. Paulo alisema, “Pa—parapanda ikilia, askari akisikia tarumbeta ikilia . . .”

¹¹⁴ Kuna askari wengi wastaafu hapa asubuhi ya leo. Wanajua maana ya kurudi nyuma. Wanajua maana ya ishara hizi mbalimbali za sauti ya tarumbeta hii. Na ikiwa tarumbeta hii haitoi sauti inayojulikana, ni kelele tupu tu, je, askari atajua je kujiandaa?

¹¹⁵ Kanisa moja likisema fanyeni *hivi*, kanisa lingine linasema fanyeni *vile*, na kanisa moja linasema fanyeni *hivi*, lingine linasema fanyeni *hivyo*, Mkristo anawezaje kujua la kufanya? Moja linasema jambo moja, na moja lingine.

¹¹⁶ Lakini nakwambia, ndugu yangu mpendwa, nitakwambia mahali pasipo na sauti isiyojulikana. Hapo ni katika Biblia, Neno la Milele la Mungu! Ni Injili. Na Injili ni Nguvu na dhihirisho la Roho Mtakatifu ikiwekwa katika matendo. Naam.

“Sauti isiyojulikana.”

¹¹⁷ Yesu akiwa amesimama duniani, anajua mahali aliposimama. Alijua Yeye alikuwa ni Nani. Akasema, “Ninao Uweza wa kutoa uhai Wangu. Ninao Uweza wa kuutwaa tena.” Hakuna mashaka kuhusu hilo.

“Ninao!” Haleluya! “Sasa ninao Uweza wa kuutoa. Ninao Uweza wa kuutwaa.” Naam, bwana. “Hakuna anayenizua Mimi.”

¹¹⁸ Mwanamume au mwanamke yeyote aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu anajua mahali wanaposimama, bila kujali kinachotukia, au ni wangapi wanasema ndio au la. Wanajua wanaposimama. Hakuna sauti isiyojulikana. Haleluya! Loo, jamani!

¹¹⁹ Mwanamume aliye nayo, mwanamke aliye nayo, loo, ni mtu aliyebarikiwa jinsi gani. Si ajabu Daudi alisema walikuwa na heri, mtu aliyebarikiwa. Mlaze juu ya meza ya upasuaji, na uchukue . . . ujariibu kukata hiyo baraka kutoka kwake, huwezi kuipata. Ni Nguvu zilizofichwa. Ni Kitu kilichofichwa, loo, lakini kipo. Kila mwanamume na mwanamke waliopata kuwa nayo, walijua wameipata. Hakuna mashaka juu Yake. Kila mtu aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, anajua alipopita mautini kuingia Uzimani; anajua mahali, saa, dakika. Kifo kilipobadilika kikawa Uzima; wakati kutokuamini kwa Biblia, kulipobadilika kukawa ni kuamini kila Neno Lake; wakati mambo ya majivuno, kiburi yalipopita; kwa Wakristo wanyenyekevu, wanajua wakati mauti yalipopita yakawa Uzima. Amina.

¹²⁰ Kila mwanaume aliyekuwa Nao, alikuwa na kitu tofauti. Ulimwengu ulilijua hilo. Kila mwanamke alikuwa Nao, alikuwa na kitu tofauti, na ulimwengu ulijua hilo. Ulimwengu unaweza kuuona. Matendo yako yanathibitisha kile ulicho. Unaweza kusema unao, lakini matendo yako yanazungumza kwa sauti kubwa sana hivi kwamba hawawezi kusikia sauti yako. Maisha yako yananena kile ulicho.

¹²¹ Samsoni, yeye alikuwa mtu aliyepagawa Nayo. Sasa, watu wengi wanajaribu kumfanya Samsoni kuwa mwenye mabega makubwa mno na mtu mkubwa mno aliyetoka nje na kuyanyanyua malango ya mji na kuondoka. Hilo si, hilo si fumbo kubwa kwangu, kuona mwanamume akifanya hivyo, mwenye mabega makubwa namna *hiyo*. Samsoni hakuwa mtu mkubwa. Maandiko yote yanamtangaza kuwa ni maskini kijitu kidogo. Naye alibarikiwa. Kwa nini? Alizaliwa hivyo.

¹²² Hivyo ndivyo unavyobarikiwa, ni wakati unapozaliwa hivyo. Si wakati kasisi fulani anapokubariki, au mhubiri fulani anapokubatiza. Lakini wakati Mungu, kwa Roho Mtakatifu, anapotoa uzao mpya, basi unazaliwa, mtoto wa Mungu.

¹²³ Samsoni aliiacha ndani yake. Na haikuwa ni Samsoni, ilikuwa ni Nguvu zilizofichwa ndani yake.

¹²⁴ Sio neno la kichawi. Sio kuusugulia mguu wa sungura nyuma ya sikio lako, kutemea mate kiatu cha farasi na kukitupa huko, huko kunafanya uchawi. Hilo silo linalomfanya mtu aishi maisha tofauti; si zaidi ya kujiunga na kanisa, ama kuandika jina lako kwenye kitabu, ama kubatizwa. Kinachomfanya mtu ni wakati Mungu, kwa kuzaliwa, anapompa Nguvu zilizofichwa, na kumbariki kwa Roho Mtakatifu maishani mwake, ndicho kinachomfanya jinsi alivyo.

¹²⁵ Samsoni, alipotoka nje kule, simba alimjia. Loo, jamani, simba alikuwa anataka kumshambulia! Kibete kidogo, chenye nywele za kipilipili, namna *hiyo*; maskini vishungi saba vya kidondoadume vikining'inia kutoka mabegani mwake. Naye alikuwa mnyonge, alikuwa mbilikimo, alikuwa kibushuti, kama vile kila mtu alivyo asiye na Mungu. Naam. Lakini, kwa ghafla, simba alipojitayarisha kumshambulia, zile Nguvu zilizofichwa zikatokea. Roho Mtakatifu akaja juu yake. Naye akamnyakua huyo simba na kumwua, kana kwamba alikuwa ni mwana-kondoo.

¹²⁶ Hapo ndipo ilipo. Mkristo hajibu kwa kupigana. Mkristo habishani juu yake. Mkristo hutulia kimya. Nazo Nguvu hizo zilizofichwa, baraka za Roho Mtakatifu zinaanza kumtendea kazi, zinajitokeza. Haleluya! Hiyo...?...

¹²⁷ Daudi alikuwa nazo. Alipocheza mbele ya sanduku la Bwana, alikuwa Nazo. Alijua alichokuwa akizungumzia, kwa hiyo hiyo ndiyo sababu hakumwogopa Goliathi. Jiwe alilokuwa nalo Daudi kwenye kombeo silo lililomwua Goliathi.

Kombeo alilokuwa nalo mkononi silo lililomwua Goliathi. Mawe aliyokuwa nayo mfukoni siyo yaliyofanya hivyo. Ilikuwa ni Nguvu zilizofichwa, ile baraka ya Mungu. Daudi alipoachilia kile alichokuwa nacho, Mungu alikitwaa na kukibariki kwa Nguvu zilizofichwa. Kwa hiyo, haikuwa Daudi, haikuwa ni lile jiwe, haikuwa ni lile kombeo. Ilikuwa ni baraka ile iliyokuwa juu ya Daudi, iliyomwua adui wa Daudi. Amina.

¹²⁸ Watoto wa Kiebrania walikuwa Nazo. Walikuwa na ujasiri. Walisema, “Mungu wetu anaweza kutukomboa kutoka kwenye tanuru ya moto. Lakini kamwe hatutaisujudu.” Hakukuwa na mashaka yoyote kwa hilo; hakuna sauti isiojulikana.

¹²⁹ Hakukuwako na sauti isiojulikana kwa Daudi, aliposema, “Je, mnataka kuniambia ya kwamba mtaacha... Mfilisti yule asiyetahiriwa kusimama pale na kuyatukana majeshi ya Mungu aliye hai?” Kasema, “Nitapigana naye mimi mwenyewe.” Amina. Hakuna mashaka. Daudi alijua mahali aliposimama.

¹³⁰ “Mungu alisema, ‘Daudi, nilikutoa katika zizi la kondoo, ulipokuwa si kitu ila mvulana wa kondoo, nami nikalikuza jina lako kati ya wanadamu, kama watu mashuhuri wa ulimwenguni.’” Nathanaeli akamtazama, kasema, “Fanya yote yaliyo moyoni mwako, kwa maana Mungu yu pamoja nawe.”

¹³¹ Hakuna mashaka. Walimjua Mungu. Walikuwa na ujuzi. Hakuna sauti isiojulikana juu yake.

¹³² Daudi akasema, “Nitakwenda kupigana naye, na leo hii nitakikata kichwa chake.” Hakuna mashaka. Si Daudi; ilikuwa ni Mungu ndani yake. Ilikuwa ni zile Nguvu zilizofichwa. Hakuna shaka hata kidogo. Yote ni hakika. Hakuna shaka.

¹³³ Wale wana wa Kiebrania walisema, “Hatutaisujudia miungu yako. Hatutaziabudu maskini dini zako baridi. Mungu anaweza kutukomboa. Lakini asipotukomboa, tuko tayari kufa.”

¹³⁴ Ndani ya ile tanuru ya moto! Nanyi mnajua lililotukia? Walipoliamini Neno la Mungu, na kuingia kwenye hiyo tanuru ya moto, Nguvu hizo zilizofichwa zilitokea. Amina. Zikawazingira pande zote, nao wakawa na ushirika. Mmoja kama Mwana wa Mungu akasimama miongoni mwao, akipeperushia mbali upepo wenye joto, na kufanya ushirika katikati ya shida kuu sana waliyopata kupitia.

¹³⁵ Na kila mwanamume au mwanamke aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, saa itakapofika, fanya uamuzi wako na umtetea Mungu, bila mashaka yoyote. Katikati ya shida, utakuwa na ushirika. Hakuna mashaka.

¹³⁶ Walimtupa Danieli katika tundu la simba. Hakuna mashaka. Akasimama pale. Alikuwa na Nguvu zilizofichwa! Sio mguu wa sungura mfukoni mwake; sio hirizi ya kuvaa shingoni mwake!

¹³⁷ Wananichefua tumbo kwa misalaba hiyo yote na hirizi, na kila kitu, Waprotestanti na Wakatoliki wote huvaa. Hakuna

nguvu ndani yao. Ni sawa kuwa nayo; bali kuiabudu jinsi mnavyoiabudu, mnaining'iniza kwenye magari yenu na kufikiri itawalinda na ajali ya barabarani, haitafaa kitu. Mkono wa Mungu ndio pekee unaoweza kufanya hivyo. Amina.

¹³⁸ Iie nyoka ya shaba ilikuwa sawa. Hakukuwa na hukumu katika hiyo nyoka ya shaba. Lakini walipoanza kumwondokea Mungu, na kumwabudu nyoka, nabii aliangamiza. Amina. Haya basi.

¹³⁹ Danieli aliingia, bila mashaka yoyote. "Mungu ana uwezo wa kunikomboa kutoka kwa simba hao." Lakini wakamtupa katika tanuru ya moto... Nami naamini wakati hao simba walipoanza kumwendea kule, wakamwalia, hiyo hapo duara ya Moto imemzunguka Danieli. Mnyama yeyote anaogopa moto, mnajua hilo. Simba hao wakarudi nyuma. Ilikuwa ni nini? Zile Nguvu zilizofichwa, zilizokuwa moyoni mwa Danieli, zilitoka na kumvika kila mahali. Ilikuwa ni zile Nguvu zilizofichwa, baraka ile ya Mungu, iliyokuwa juu ya maisha ya nabii huyo, ambayo ilimfunika kwa Moto uwakao; kama kule chini Dothani siku ile Gehazi alipotazama na kuona kile kilichokuwa kimemzunguka Eliya: Malaika wa Moto, magari ya Moto. Huko, Nguvu hizo zilizofichwa zilikuwa karibu na Danieli.

¹⁴⁰ Petro na Yohana, walipopita katika lango litwalo Zuri, Bwana alizungumza nao juu ya kiwete aliyekuwa amelala pale. Hakukuwako na mashaka. Hawakuwa na elimu yoyote. Hawakuwa na... Hawakuwa hata wafuasi wa kanisa. Hawakuwa wa madhehebu. Lakini hakukuwako na mashaka juu ya ujuzi wao. Walikuwa na uhakika. Hawakuwa na pesa. Hawakuwa na uanachama. Hawakuwa na elimu. Lakini Petro akasema, "Nilicho nacho, nakupa. Katika Jina la Yesu Kristo, simama na uende."

¹⁴¹ Walikuwa na Nguvu zilizofichwa. Walivaa kama watu wengine. Walitembea mtaani. Walikula kama watu wengine. Lakini walikuwa na baraka ndani yao, ambayo iliwapa uhakika wa kujua mahali walipokuwa wamesimama. Kasema, "Sina elimu yoyote. Mimi si mfuasi wa kanisa lolote. Sijui theolojia yoyote. Sina pesa zozote. Kitu pekee nilicho nacho, nitakupa wewe kama utakikubali."

Akasema, "Ni nini?"

¹⁴² Alisema, "Katika Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama uende." Hakuna mashaka. Sio "simama na ujaribu, uone kama unaweza kuusogeza mguu wako." Sio "simama ujaribu, uone kama utapata nafuu." Lakini, "Katika Jina la Yesu Kristo, simama uende sasa." Haya basi.

¹⁴³ Sauti isiyojulikana ni... ikitoa sauti isiyojulikana, itakuwaje? Loo, jamani.

¹⁴⁴ Stefano alikuwa na kiasi kikubwa sana cha hizo baraka ndani yake, kasema, walipokuwa wakimpiga Stefano kwa mawe.

Loo, jamani! Alikuwa na kiasi kikubwa cha baraka hizo ndani yake, kiasi kikubwa cha hizo Nguvu zilizofichwa, mpaka Stefano akawa ni mtu mwingine, akatazama juu na kumwona Yesu amesimama mkono wa kuume wa Mungu; na kamwe hata hakuhihi bongwe lilipompiga kichwani.

¹⁴⁵ Mbona, ninaweza kumwona Stefano pale. Akapiga magoti. Adui zake, wakimtemea mate, na chochote kile, na kumpiga kwa mabonge. Alisimama, na kuangalia Mbinguni. Naye akasema, “Baba, usiwahesabie dhambi hii. Nawasamehe Baba.” Baraka nyingi sana ndani yake! Ilikuwa? Nawaambia, ndipo Mbingu zikafunguka. Maskini huyo Roho, aliyekuwa juu yake, alifungua njia kupitia mawinguni, kupitia kwenye nyota, kupitia ukungu, mpaka akamwona Yesu amesimama mkono wa kuume wa Mungu. Akasema, “Tazama, naona Mbingu zimefunguka.”

¹⁴⁶ Ndugu, ni afadhali niwe nayo kuliko elimu yote, pesa zote mnazoweza kulundika mbele yangu. Elimu yangu yote, nitaiacha hapa. Theolojia yangu yote ya kiakili, nitaiacha hapa. Utajiri wangu wote, nitauacha hapa. Lakini zile Nguvu zilizofichwa, kitu kile kilichofanya uhakika wa Injili, kitakuchukua mpaka Mbinguni, na kukupitisha katika mabonde ya uvuli wa mauti. Amina.

¹⁴⁷ Alijua alichokuwa akizungumzia. Kasema, “Naona Mbingu zimefunguka.” Alikuwa na baraka. Alikuwa na Nguvu zilizofichwa. Wala hakuhihi mabonge yoyote baada ya hapo. Walikuwa wakimpiga mawe kichwani. Kumpiga upande mmoja, mwingine. Maskini Stefano alikuwa kama mtoto mchanga, amelazwa mikononi mwa mama yake, na mwa Mungu, Naye akampembeza alale kifuani Mwake.

¹⁴⁸ Biblia haikusema Stefano alikufa. Biblia ilisema, “Stefano akalala.” Mungu aturehemu! Ndugu, hiyo ndiyo ninayotaka mwishoni mwa safari. [Ndugu Branham anapiga makofi mara mbili.] Akamweka kifuani mwa Mungu na kumpembeza akalala, akasema, “Ona, mwanangu, ninakokupeleka.”

¹⁴⁹ Alikuwa na baraka. Alikuwa na Nguvu zilizofichwa. Sio mguu wa sungura; si hirizi mfukoni mwake; lakini kitu fulani nafsini mwake, ambacho kilimbadilisha na kumfanya mtu tofauti.

¹⁵⁰ Paulo alisema, “Maisha ninayoishi sasa.” Ilionyesha aliishi mengine tofauti, wakati mmoja. “Si mimi, bali Kristo aishiye ndani yangu,” alisema. Naam.

¹⁵¹ Yohana, mfunuzi, alikuwa na sauti fulani kwa sauti yake. Alimpenda Bwana. Alilala kifuani Mwake. Alikuwa na ushirika pamoja na Yesu. Aliishi karibu miaka mia moja. Alifanya miujiza na ishara na kuona maono.

¹⁵² Basi walipofanya hivyo, walisema, “Yeye ni mchawi.” Kwa hiyo wakamchukua na kumchemsha, saa ishirini na nne, katika sufuria kubwa ya grisi. Mnajua nini? Nguvu hizo zilizofichwa

zikatokea. Nguvu zile zilizofichwa, zilizokuwa moyoni mwake, zilimfunika pande zote. Nao walipoangalia kwenye kile chungu cha grisi, baraka hiyo ilikuwa juu ya Yohana. Nao wakamtoa kwenye grisi, pasipo hata na harufu ya grisi juu yake. Nao wakasema, “Yeye ni mchawi. Yeye ni mpiga ramli. Yeye ni Beelzebuli.”

¹⁵³ Kila mwanamume au mwanamke ambaye amewahi kujaribu kumwishia Mungu anashutumiwa kwa mambo maovu. “Yeye ni mchawi. Aliiroga grisi.” Alikuwa na Nguvu nyingi sana za Mungu ndani Yake, nyingi sana. . . Si uchawi. Lakini ilikuwa ni nini? Nguvu za Mungu zilizofichwa zilizokuwa ndani yake. Alionekana kama mwanadamu. Alikula kama mwanadamu. Alilala kama mwanadamu. Alilia kama mwanadamu. Alikuwa mwanadamu. Lakini Mungu alikuwa ndani ya mtu Wake. Baraka zilikuwa ndani ya huyo mtu.

¹⁵⁴ “Heri mtu,” alisema Daudi. Hakuna mashaka kwake. Mtu huyo anajua anachozungumzia. Sijali ulimwengu unasema nini, kile unachosema juu yake, kujaribu kumkasirisha sana, hatakasirika. Sijali ni kiasi gani unamsengenya, hatalizingatia. Ataendelea, maana ana baraka humu ndani. Atakuombea. Hiyo ni kweli. Unaweza kufanya chochote duniani, yeye hajali hata kidogo. Hatawasengenya majirani zake, na kwenda huku na huko na kuchochea matata. Atakuwa mpatanishi. Atafanya kila awezalo, kwa maana yeye ni mtoto wa Mungu. Heri mtu huyo. Naam.

¹⁵⁵ Wakati wapentekoste walipopanda kwenda Pentekoste walikuwa ni watu tu wakati walipopanda kule. Lakini kwa ghafula, wakiwa pale juu, waliogopa. Walikuwa wamefunga madirisha, milango imefungwa. Waliogopa mateso. Walikuwa washiriki wazuri wa kanisa, kufikia wakati huo. Walikuwa wamebatizwa kwa maji, hadi wakati huo. Ila hawakuwa na Nguvu hizo zilizofichwa. Hawakuwa na uhakika huo.

¹⁵⁶ Mmoja wao akasema, “Ikiwa Ndiwe. . . Acha niweke mikono yangu ubavuni Mwako. Acha niweke vidole vyangu kwenye alama za misumari, mkononi Mwako.”

¹⁵⁷ Mwingine akawaambia wale wanawake, “Loo, ni ujinga! Hamkuona chochote.”

¹⁵⁸ Lakini walipopanda hizo ngazi na kupanda ghorofani, mara sauti ikaja kutoka Mbinguni, nazo Nguvu zilizofichwa zikashuka. Zikaingia ndani yao. Baadaye walikuwa huko nje mtaani, . . . -kishangilia—wakishangilia na kumsifu Mungu, wakiihubiri Injili, wakimtukuza Mungu. Walikuwa na Nguvu zilizofichwa. Walikuwa na Nguvu ambazo ulimwengu haukujua lolote kuzihusu.

¹⁵⁹ Sasa ni vile vile. Sauti isiyojulikana; usiamini sauti isiyojulikana. Injili haina sauti isiyojulikana.

¹⁶⁰ Wasema, “Ndugu Branham, ninaamini kanisa langu linahubiri Injili.” Vema.

¹⁶¹ Yesu alisema, “Sasa nitawapa jambo fulani la kuamini.” Akasema, “Enendeni ulimwenguni mwote sasa mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe. Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa. Na. . .” Amina! Loo, najisikia vizuri. “Na” ni kiunganishi. Usisimame hapa, “kuhubiri Injili.” “Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Hakuna sauti isiyojulikana. Ni Injili. Amina.

¹⁶² Wanatoa pepo. “Kwa Jina Langu watatoa pepo.” Hiyo si sauti isiyojulikana. Injili ilisema hiyo ndiyo sauti iliyo kwenye kengele. Utukufu! Haleluya! Loo, jamani! Hiyo ndiyo sauti ya kengele, wanapotoa pepo.

¹⁶³ “Watasema kwa lugha mpya.” Simaanishi sauti isiyojulikana sasa. Wanazungumza kwa ujuzi, kwa ufunuo. Walikuwa na karama halisi ya kunena kwa lugha. Kuna kitu kinachotendeka wanapofanya hivyo. Hiyo siyo sauti isiyojulikana. Hiyo si sauti ya kutoamini, hata kidogo. Ikiwa ni kupiga makelele sana, kama tunavyoona mara nyingi, huko ni kutokuamini. Lakini unaponena kwa Maneno, kwa tafsiri, kwa ufunuo, haleluya, hiyo ni sauti ya kengele ya Injili. Sio sauti isiyojulikana.

¹⁶⁴ “Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.” Hiyo si sauti isiyojulikana.

¹⁶⁵ Enyi watu wapendwa, mlio wa Church of Christ, huko nyuma, mnasema, “Hilo ni la ibilisi.” Kweli? Basi Biblia ni ya ibilisi. Mnaona?

¹⁶⁶ Biblia ilisema, “Wataweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya. Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari.” Si sauti isiyojulikana.

¹⁶⁷ Iweni waangalifu, mumesikia theolojia nyingi za kanisa. Ni sauti zisizojulikana. Haiendani na Biblia. Paulo alisema, “Ikiwa—ikiwa baragumu haitoi sauti inayojulikana, tunawezaje kujua ni nani atakayejiandaa kwa vita?” Naam, bwana. Loo, jamani!

¹⁶⁸ Yesu alisema, “Mambo haya niyafanyayo ninyi nanyi mtayafanya, hata makubwa zaidi, kwa maana Mimi naenda kwa Baba Yangu.” Hakuna sauti isiyojulikana; hata kidogo.

¹⁶⁹ Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, katika Matendo 2:38, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Hiyo si sauti isiyojulikana.

¹⁷⁰ Hapakuwapo na mahali katika Biblia, popote pale, kutoka Mwanzo hadi Ufunuo, ambapo Mungu alipata “kumnyunyizia” mtu. Hiyo ni sauti isiyojulikana. Hapakuwapo na mahali ambapo mtu yeyote alibatizwa kwa njia nyingine yoyote

isipokuwa katika Jina la Yesu Kristo. Kitu chochote kinyume ni sauti isiyojulikana.

¹⁷¹ Soma Biblia. Hivyo ndivyo Injili imefanyizwa. Hii ndiyo Mbegu. Mbegu itazaa tunda Lake. Whiu! Kidogo kuna joto, sivyo? Lakini ni nzuri.

¹⁷² Aina ya Moto tunaohitaji ni “Roho Mtakatifu pamoja na Moto,” kuchoma tamaa za mwili na ukanisa kutoka kwetu, kuturudisha kuwa wana na binti za Mungu; ambapo theolojia hii ya kiakili na yale mnayojifunza katika seminari huku nje, na kadhalika, yatapita, naye Mungu anaweza kuingia moyoni mwako. Hilo ndilo muhimu.

¹⁷³ Sio kama utasema “Salamu Maria,” ama sio kama utashuka na kuikariri Kanuni ya Imani ya Mitume kwenye kanisa la Kiprotestanti; hilo halina uhusiano wowote Nalo, hata kidogo.

¹⁷⁴ Yesu alisema, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hataingia katika Ufalme.” Amina. Si sauti isiyojulikana, hata kidogo.

¹⁷⁵ Wakati Eliya alipopanda kule . . . Tazama, hebu niwaonyeshe jambo fulani. Elisha alipokuwa akimwangalia Eliya, anapanda juu na kumwangalia. Kasema, “Unataka nini?” Mfano wa Kristo na kanisa.

Akasema, “Nataka kuona kitu fulani.” Kasema, “Unataka nini?”

¹⁷⁶ Akasema, “Nataka sehemu maradufu ya Roho yako unapoondoka.” Hiyo ilikuwa njaa. Hiyo ilikuwa theolojia. Hayo yalikuwa ni mambo ya akili. Alikuwa akiyaonea njaa. Nia yake iliyataka. Nafsi yake ilikililia. Hiyo haimaanishi kuwa alikuwa nacho.

¹⁷⁷ Eliya akasema, “Umeomba jambo gumu. Lakini ukiniona ninapoondoka, sawa, itakuja kwako.” Ndugu, alimnazama nabii huyo, kila hatua aliyofanya.

¹⁷⁸ Ndipo wakati wito huo wa mwisho ulipokuja, naye Eliya akaitwa apae Juu, akaonekane Mbele za Mungu, Mungu alimteremshia gari limbebe. Utukufu! Loo, jamani! Akamshushia gari, pamoja na farasi wa gari. . . farasi wa Moto, na gari la Moto. Kasema, “Mtumishi wangu mpendwa, ingia! Imefanywa vema.”

¹⁷⁹ Kasema, “Vema, Elisha, naona unanitazama.” Anavua koti lake na kulirusha nyuma.

¹⁸⁰ Akaokota koti lile lile na kulivaa. Hamna mashaka. Akateremka mtoni! Haleluya! Alikuwa ameona kile Eliya alichofanya. Akamfungulia, apate kuvuka *huko*. Akasema, “Kama Yeye angali ni yeye yule, na Roho Wake yuko juu yangu, utafunguka tena.” Hakuna mashaka. Akalizungusha hilo pande zote, na kusema, “Yu wapi Mungu wa Eliya?” Nayo bahari ikagawanyika huku na huko, naye akavuka. Je, mliona? Haikumlazimu kwenda kwenye shule ya manabii kupata

elimu yoyote. Utukufu! Whiu! Hamna elimu ndani ya mvulana huyo, naye akatembea! Theolojia ya kiakili ilikuwa imekwisha. Alikuwa nayo nafsini mwake. Mwangalieni, alifanya kama Eliya alivyofanya.

¹⁸¹ Yesu alisema, “Kikombe kile kile ninachokinywea, mtakinywea. Na ubatizo ule ule ninaobatiziwa, mtabatiziwa. Na mambo yale yale nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya.” Alifanya nini? Alinena kwa lugha, akatoa pepo, akahubiri Injili, akawaponya wagonjwa. Jambo lile lile alilofanya, sisi tunaweza, pia. Na mwishoni mwa siku zetu, kama Yeye alivyofufuka katika wafu, vivyo hivyo na sisi tulio ndani Yake.

¹⁸² Siwezi kumwamsha mvulana wangu, asubuhi. Anaonekana kana kwamba mchana wake na usiku umebadilishana. Nilisema, “Billy, hutawahi kuwa na faida yoyote ukilala hapo namna hiyo. Amka. Ikiwa hutafanya chochote zaidi ya kutoka nje na kusugua meno yako, na kwenda nje kwenye kitalu, uliangalie gari lako, kisha urudi ndani na kuketi chini, usome. Usilale kitandani; sio vema, uvivu.”

¹⁸³ Mungu awarehemu Wakristo hawa wenye mioyo yenye uvivu, kuwa wasio na faida; wanajua mengi sana kulihusu, na kuwaambia wengine machache sana juu Yake.

Akasema, “Baba, siwezi kabisa kuamka mapema.”

¹⁸⁴ Nikasema, “Angalia, Billy, moja ya siku hizi, hutakuwa na baba wa kukushughulikia. Baba atakuwa ameondoka, moja ya asubuhi hizi, utaingia chumbani na kuangalia, labda Baba atakuwa amelala hapo, utamtikisa, lakini hataamka.” Nikasema, “Ndipo watanishusha chini, maskini kanisa hili la kale kwenye jeneza. Utapita, lesa yako mkononi mwako, ukilia, uangalie chini, useme, ‘Huyo hapo maskini baba yangu, laiti ningelimsikiliza.’” Nikasema, “Lakini kumbuka, Billy, sikuzote nimekuwa mtu wa kuamka mapema.”

¹⁸⁵ Haleluya! [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]... baragumu iliyobarikiwa Italia, nitatokea katika ule ufufuo wa kwanza. Ninaamini katika kuamka mapema, (haleluya), siku moja tukufu, kwa neema ya Mungu. Ninaamini Injili hii ninayohubiri. Ninaamini ni Ukweli mtupu.

¹⁸⁶ Vazi la Elisha halina sauti isiyojulikana. Hakuna sauti isiyojulikana.

¹⁸⁷ Mbunge Upshaw... Hapakuwepo na sauti isiyojulikana wakati Roho Mtakatifu aliponiambia kule juu, kabla madaktari hata hawajapata ameba. Hakukuwa na sauti isiyojulikana, wakati daktari aliposema kwamba nilikuwa nafa, na iliku-... Mungu aliniponya. Hakukuwa na sauti isiyojulikana. Hakukuwa na sauti isiyojulikana, kule Green's Mill usiku ule, wakati Malaika wa Bwana aliponijia, akasema, “Kwa sababu hii ulizaliwa ulimwenguni.” Hakuna sauti isiyojulikana!

¹⁸⁸ Nikaenda na kuzungumza na wahubiri fulani kuhusu jambo hilo. Wakasema, “Billy, ulikuwa na jinamizi.” Lakini kumekuwa na watu milioni moja walioletwa kwa Kristo. Hakukuweko na sauti isiyojulikana. Hiyo ilikuwa ni sauti ya Mungu ikizungumza na maskini hohehahe. Hakuna sauti isiyojulikana. Loo, kamwe siwezi kuhubiri nikiwazia jambo hilo.

¹⁸⁹ Nilikuwa nikimwambia mke wangu, wakati fulani uliopita. Huenda nililisimulia hapa awali. Mnajua asili ya familia yangu. Nampenda baba yangu. Ametuacha. Alikufa mikononi mwangu, akiomba. Lakini alikunywa pombe. Familia yangu yote ilikunywa pombe. Walifanya mambo makubwa, yanayoumiza; hata hivyo, ni aibu kwa jamii. Ndugu zangu hunywa pombe; sio kwa sababu ninataka wafanye hivyo. Ninawalilia, ninawaombea, chochote kile.

¹⁹⁰ Ilikuwa, kabla Mungu hajaniita, ningekuwa nimesimama mtaani, nikizungumza; mtu, wao... Kwa sababu ya lile jina, wangeninii, loo, “Branham? Looo!” wanaondoka. Mtu mwingine anapitia hapo, anamwalia mtu, anasema, “Mwache!” Vema, basi wangeondoka. Wasingezungumza nami.

¹⁹¹ Nilimwambia mke wangu, hivi majuzi, “Sasa inanilazimu kuponyoka niende msituni mahali fulani na kujificha, kuwakwepa watu, kutoka duniani kote, wanaokuja.”

¹⁹² Ni nini ilileta hayo? Kwa maana nilisoma sana? Kwa sababu nilijifunza theolojia? Kwa kuwa nina elimu? Kwa sababu nilijiunga na kanisa fulani? Hapana. Hiyo ingekuwa sauti isiyojulikana.

¹⁹³ Lakini kitu fulani kilitoa sauti siku moja, chini moyoni mwangu, si akilini mwangu, moyoni mwangu. Mungu akaingia. Imekuwa nzuri tangu wakati huo. Hiyo ni neema ya ajabu.

¹⁹⁴ Hivi majuzi nilishangaa, zaidi ya chochote ambacho kimetokea kwa muda mrefu. Mimi napenda maumbile sana. Mnajua nayapenda. Ninawapenda wanyama. Nafikiri tu wao ni wa ajabu. Nilikuwa nimeketi mlangoni pangu. Ndugu Leo na Gene walikuwepo. Na Ndugu na Dada Wood walikuwa kule chini. Na maskini Billy Gillmore, muuza maziwa, alikuwa amesimama pale. Na saa nne asubuhi, kitu fulani kikashuka barabarani, kikichechemea, kikiukokota mguu nyuma yake. Kikaingia langoni pangu, na kupanda vipandio vyangu. Ilikuwa ni maskini oposamu, saa nne mchana.

¹⁹⁵ Wao ni vipofu wakati huo wa mchana. Wao ni vipofu, wote, mchana. Wao ni mnyama wa usiku atembeaye usiku. Wanawinda, na kuwinda kote, na kupata riziki yao usiku. Nyote mnajua hilo. Oposamu ni mnyama anayeliwa.

¹⁹⁶ Naye akaingia langoni. Nikatoka kwenda kumlaki huyo oposamu. Nikachukua reki. Nikawazia, “Ajabu! Anaweza kuwa ni kipofu. Ni kitu gani kinachomfanya atende na kuyumbayumba namna hiyo?” Nikaweka reki juu yake. Naye

akageuka na kunitazama, akaguna. Nikawazia, “Kuna kitu kisicho cha kawaida.”

¹⁹⁷ Ndipo ikatokea niliangalia chini mfukoni mwake. Oposamu ni kitu kimoja, mbali na kangaruu, wapo wawili tu ambao wana mfuko wa kuwabebea watoto wao. Na katika mfuko wa oposamu, alikuwa na watoto wadogo wanane ama tisa wasio na nywele mle ndani. Naye mbwa alikuwa amemshika, labda au gari; akamvunja mguu, mfupa wa bega lake. Nzi wa kijani kibichi kote mwilini mwake; funza masikioni, na kadhalika. Naye huyu hapa, akichechemea namna hiyo. Ndipo akaguna kwa sababu alidhani nilikuwa nikitaka kuwachukua watoto wake.

¹⁹⁸ Nikasema, “Oposamu huyo ana umama mwingi zaidi juu yake kuliko wanawake wengi, hasa mwanamke huyu aliyemtupa mtoto wake mchanga mtoni, hivi majuzi, kumwondolea mbali.” Nikawaambia Gene na Leo, wanaoketi pale nyuma, nikasema, “Njoni hapa nami nitawafundisha mahubiri.” Nikasema, “Angalieni maadili ya mwanamke huyu. Angalieni maadili ya mama huyu. Ni mnyama bubu, lakini ana umama mwingi kuliko asilimia arobaini ya wanawake wa Marekani.” Kweli. Nikasema, “Ana takriban saa moja tu ya kuishi, anavyoonekana, lakini atatumia saa hiyo kupigana apate kuwalinda hao watoto. Na wanawake hawa wanatoka hapa nje na kuzaa watoto, na kuwakaba roho, na kuwazamisha majini, na kuwatupa motoni, na kadhalika; wabaya kuliko mbwa, wabaya kuliko wanyama.”

¹⁹⁹ Maskini huyu mama asingesubiri. Hata asingesimama, kidogo. Alikwenda moja kwa moja mlangoni pangu; na, huku amechoka sana, akalala hapo. Tukajaribu kumwinua. Alikuwa amekwisha. Alikuwa bado anaguna, akiteseka sana.

²⁰⁰ Bibi Wood akaja, na Bw. Wood na hao wengine, kasema, “Ndugu Branham, ninaamini jambo la kibinadamu la kufanya, ni, kumwua huyu oposamu. Maskini hao watoto wachanga watakufa njaa.” Kasema, “Ndilo jambo pekee unaloweza kufanya, ungelifanya.”

²⁰¹ Mtu mwingine alikuja na kusema, “Ndugu Branham, si umwue huyu oposamu?” Kasema, “Mwue. Yuafa.” Kasema, “Amelala pale akiteseka.” Akasema, “Wachukue hao watoto uwaue. Wangekuwa afadhali zaidi.” Kasema, “Hawana nafsi. Ni mnyama bubu tu, mnyama tu.” Kasema, “Maskini hawa watoto wadogo watakufa kwa njaa. Maskini huyo mama aliyelala hapo, nao hao watoto wachanga wakinyonya hayo maziwa kutoka kwake, nawe unajua hali aliyokuwa nayo,” kasema, “watakufa.”

²⁰² Kasema, nikasema, “Ni kweli, mimi ni mwindaji, lakini mimi si mwuaji.” Nikasema, “Ninapenda kuwinda, lakini siui tu ili kuua. Huyo ni mwuaji.” Hiyo ni kweli. Siui chochote nisichoweza kula, au kitu nisichoweza kutumia, au kitu cha kuharibu. Si kuua kiholela; huyo ni muuaji. Nisingeweza kufanya hivyo. Kamwe nisingeweza kufanya hivyo.

203 Na nilijua kwa busara, katika milki ya kiakili, kwa njia sahihi ya kuwazia, jambo la kibinadamu lingekuwa, kufanya, litakuwa ni kumwua huyu oposamu na hao watoto wachanga. Huyu oposamu alikuwa yuafa, hangeweza kurudiwa na fahamu tena. Na hao watoto wachanga wangekufa kwa njaa. Nao wakinywa maziwa hayo yaliyoganda kutoka kwa mama yao, pengine wangekufa katika dhiki. Jambo bora la kufanya ni kuwaondoa katika dhiki yao. Hilo lilikuwa ndilo jambo la busara. Lakini kitu Fulani *hapa* chini kisingeniruhusu kufanya hivyo.

Umati wa watu ukaanza kuja. Nilipigiwa simu, nikaondoka.

204 Usiku huo, mimi pamoja na Ndugu Wood tulikuwa tukiendesha gari barabarani, na Dada Wood pamoja na mke wangu. Tukishuka, kutoka huko juu kuelekea Scottsburg, ambako nilikuwa nikijaribu kuipumzisha akili kidogo. Ndugu Wood akasema, “Unamwona maskini yule mtoto wa mbwa huko nyuma barabarani?” Kasema, “Atakanyagwa.” Nikalizungusha gari langu na kurudi. Tukamchukua maskini jamaa huyo.

205 Alikuwa amejaa viroboto na chawa, nao upele umemla. Vema, jambo la busara la kufanya lingekuwa nini? Kumwua. Nisingeweza kufanya hivyo. Nikamleta maskini jamaa huyo nyumbani, nikajichukulia poda ya viroboto na kumnyunyizia, nikajichukulia dawa ya upele; nikampa chakula kizuri kinachofaa. Nikamficha huko juu, nikijaribu kumfanya maskini jamaa huyo apate afya. Anataka kuishi.

206 Kuna kitu kuhusu uhai ambacho ni halisi. Usiige Ukristo. Pata Uzima! Ishi! Sio lazima ujifanyie vita tu huku, useme, “Vema, mimi ni Mkristo, sistahili kufanya *hili*; sikupaswa kufanya *lile*.” Ishi! Kuna Mmoja anayekujali.

207 Usiku huo, saa nne na nusu au saa tano, maskini huyo oposamu alikuwa bado amelala bila ufahamu; nzi wa kijani kibichi kila mahali, bega limevunjika; amelala pale akiteseka, akifa.

208 Muda mrefu, baadaye, Billy akaingia. Huyu hapo huyo oposamu amelala, amelala kule nyuma, hao watoto wachanga wakijaribu kunyonya maziwa kidogo, zaidi, kutoka kwake, uhai ukitoka kwa huyo mama. Bado alikuwa anaguna vibaya sana. Angejaribu kuamka, wala asingeweza. Angejaribu kuamka, wala asingeweza.

209 Nisingeweza kumwondosha maskini oposamu huyo akilini mwangu. Niliwazia, “Mungu, imenipasa kuingia na kuchukua bunduki na kumuua huyo oposamu, lakini siwezi kufanya hivyo. Kuna nini, Bwana?” Nikatembea huku na huku sakafuni.

210 Kukapambazuka. Maskini yule oposamu amelala pale. Nikarudi, nikawazia, “Ee Mungu, huyo hapo, jua lile kali, amelala papo hapo mlangoni pangu.” Nikaanza kurudi nyuma sakafuni.

211 Roho Mtakatifu mbarikiwa akanisimamisha, akasema, “Ulimwita mama. Ulimtetea, kwamba ni mama halisi. Nami nilimtuma nyumbani kwako akaombewe, nawe unamwacha alale hapo kama mwanamke mlangoni pako.”

212 Nikasema, “Mungu, msamehe mtumishi wako mjinga.” Nikatoka pale na kusema, “Mungu, ikiwa—ikiwa una huruma vya kutosha kumshughulikia mnyama bubu, ambaye amekuwa mama vya kutosha kuwalea watoto wake, kutuma huyu oposamu mjinga mlangoni pangu apate kuombewa, Ee Mungu, mponye huyu oposamu. Katika Jina la Yesu, ninaomba.”

213 Maskini huyo oposamu akageuka na kunitazama; akasimama kwa miguu yake, akawachukua watoto wake wachanga na kuwaingiza mle ndani. Kana kwamba kuinamisha kichwa chake, na kusema, “Asante.” Naye akaelekea msituni, akishangilia. Anajua mengi zaidi kuliko wahubiri wajuavyo, wakati mwingine. Atafuata uongozi wa Roho Mtakatifu. Ikiwa Mungu anaweza kumshughulikia oposamu, ni kiasi gani angeweza kumshughulikia mwanadamu, kama tu wangeninii...?...Hakuna sauti isiyojulikana juu ya hilo. Mungu huwatumia wanyama kufundisha huduma. Hakika huwatumia.

214 Alimtumia nyumbu, wakati mmoja, kumkemea mhubiri aliyerudi nyuma.

215 Mtakatifu mkuu Francis wa Assisi, ambaye ninyi Wakatoliki mnadai alikuwa Mkatoliki, lakini hakuwa. Alilipinga kanisa Katoliki vikali kama nifanyavyo mimi. Lakini hapakuwapo na kanisa lingine katika siku hizo, kwa hiyo wakamchukua na kumwita mtakatifu. Alipotoka akaenda mtaani, kuhubiri Injili ii hii ninayohubiri sasa, ndege walikuwa wakipiga kelele mitini. Akasema, “Dada zangu wadogo, nitahubiri Injili ya Yesu Kristo. Tulieni wakati nikihubiri.” Na kila ndege akafunga mdomo wake.

216 Hii si sauti isiyojulikana. Tunaishi katika Uwepo wa Bwana Yesu Kristo. Baraka Zake ziko hapa.

217 Mungu ambaye angeweza kufanya ndege itue kule chini, na kuizuilia isiondoke kwa ajili ya mwanamke mweusi maskini, asiye na elimu, ambaye hakujua ABC zake, kumponya mvulana wake mwenye ugonjwa wa zinaa. Mnaijua hiyo hadithi.

218 Mungu, ambaye angeweza kunena na oposamu mjinga, wakati kuna wahubiri katika mji huu ambao wangeucheka uponyaji wa Kiungu; watu ambao wangeinua pua zao na kusema nilikuwa “kichaa,” kwa sababu niliufundisha. Naye Mungu akishughulika na oposamu mjinga, kwa sababu alikuwa mama, kwa sababu aliwapenda watoto wake, kwa sababu alikuwa tayari kufa kwa ajili yao. Mungu yeye yule!

219 Tumetumwa hapa duniani kwa ajili ya mambo tofauti. Wengine wametumwa kuhubiri Injili. Wengine wametumwa

kutabiri. Wengine wametumwa kuomba maombi ya imani. Wengine wana karama za uponyaji.

²²⁰ Naye Mungu yeye yule aliyenena kule chumbani mwetu usiku ule, ama hapa chini kwenye... nikiendesha gari katika ono lile, na kuniambia Ndugu Bosworth alikuwa amelala kule karibu na kufa, huko Afrika Kusini. Naye Roho Mtakatifu akafika kabla ya telegramu hapa, saa ishirini na nne. Mungu yuyo huyo, Mungu yuyo huyo alikuja, kwa heshima ya uaminifu. Ee Mungu, ibariki mioyo yao.

²²¹ Uaminifu! Ningetoa tone la mwisho la damu yangu kwa mwanamke aliye mweusi sana au wa manjano sana katika ulimwengu huu, ambaye angetaka kuishi mkweli kwa mumewe. Ningemia, kama vile ningemia mke wangu mwenyewe. Ninamheshimu, kama mama.

²²² Unafikiri Yesu Kristo alifanya nini? Na kwa nini usi—usiwe mwaminifu Kwake, na kuacha ubinafsi wako, kutojali kwako? Je, huwezi kuliacha kanisa lako, vitu vidogo vidogo, na uje Kwake na kuwa mwaminifu?

²²³ Maskini oposamu huyo mjinga, naye Roho Mtakatifu... Nami huko juu likizoni, hata sikuomba vya kutosha, na maskini mama oposamu huyo aliyelala mlangoni pangu. Wakati jua lilikuwa kali, alilala hapo kwa uaminifu. Usiku ulipofika, macho yake yangefunguka, angeweza kuona. Lakini Roho Mtakatifu asingemwacha aende zake. Alilala hapo usiku kucha. Asingeweza kuamka.

²²⁴ Na halafu, asubuhi na mapema, akionyesha alikuwa amelala pale kama saa ishirini na nne, akingoja zamu yake ya kuombewa, kwa maana alikuwa ni mnyama. Ndipo Roho Mtakatifu aliposema, “Nenda huko nje ukamwombee,” Mungu wa Mbinguni akamponya.

²²⁵ Haraka akawakusanya watoto wake wadogo mfukoni mwake, kisha akanitazama tena, kwa macho ya huzuni sana ambayo nimewahi kuona, kana kwamba kusema, “Asante, bwana mwema.” Naye huyo akaenda zake barabarani.

²²⁶ Alipita nyumba zingine nne, zilizo karibu na barabara kuliko yangu, apate kuingia langoni. Moja, mbili, tatu, nne; ya tano akaingia, J-e-s-u-s. [Kiswahili: Y-e-s-u—Mh.] akashuka langoni. Hakungojea huko nje vichakani. Hakungojea kivulini. Yeye alishika njia kwenye jua kufikia mlangoni pangu. Akalala pale, kwa subira (bila kunguruma, bila kunung'unika), akingojea zamu yake ya kuombewa.

²²⁷ Ndipo basi nilipomtii Roho Mtakatifu, Mungu akairejesha afya ya huyo oposamu. Akawachukua watoto wake na kurudi katika makazi yake. Hakuna sauti isiyojulikana. Mungu, anayehesabu manyoya katika mbawa za ndege, anajua mahali kila mmoja wayo ulipo. Mungu anayezihesabu nywele za kichwa chako; Mungu apandaye juu ya mbawa za asubuhi; Yeye

aliyeziumba mbingu na nchi, anajua kila kiumbe na kila mtu. Yeye ni Mungu. Hili ni Neno Lake. Mbingu na nchi zitapita, lakini Hili halitapita kamwe. Usidanganywe na mafundisho ya wanadamu. Mwamini Mungu, upate kuishi.

Na tuombe!

²²⁸ Baba wa Mbinguni, katika Jina la Bwana Yesu, Mwanao mpendwa; hakuna sauti isiyojulikana, hakuna mashaka kuhusu hili. Yeye ni Mwana wa Mungu. Amezaliwa na bikira. Alikuwa hapa chini ya Nguvu za Mungu. Alikuwa hapa kupitia bikira Mariamu.

Aliteseka, akamwaga damu na kufa, chini ya Pontio Pilato. Walipoweza, walimtoa, Wayahudi wakamsulubisha, na kumkana yule Mwenye Haki. Na imeandikwa, “Kwa nini mataifa wanafanya ghasia, na watu wanawazia ubatili?”

²²⁹ Ee Mungu, kwa kweli, kwa kuunyosha mkono Wako kuponya, ili ishara na maajabu yatendeke katika siku za mwisho, kuthibitisha kwamba hii ni mvua ya masika na ya vuli. Nguvu za Mungu ziko hapa. Mwana aliangaza kwenye Siku ya Pentekoste, juu ya watu wa Mashariki. Anaangaza Magharibi sasa. Waliidhihaki na kuifanyia mzaha, na kusema ilikuwa imani ya kujibunia, na kuwaita “wachawi, na wapiga ramli, na wasioamini,” na hata kuwaua, wakawateketeza kwenye nguzo na kuwatupa katika mafuta. Lakini Wewe ulikuwa pamoja nao, ili kuwaokoa.

²³⁰ Wewe uko hapa leo hii. Uko hapa, kwa ajili ya saa ya kumalizia, hata kwa ajili ya baraka kubwa zaidi, “kwa maana mvua ya masika na ya vuli inafaa kuja pamoja.”

²³¹ Na sasa, Baba, kama kuna mashaka yoyote katika tukio la mtu yeyote, katika chumba hiki; ninaomba, Baba, katika saa hii, wataielekeza imani yao, si kwa njia ya kuwazia ya kiakili, si kwa hoja za mafundisho ya wanadamu, bali kwa kuliadini Neno la Mungu, hata Uzima wa milele. Baraka hizi tunaomba katika Jina la Yesu, Mwanao.

²³² Huku vichwa vyetu vimeinamishwa, sijui kama kuna mtu hapa ndani sasa, ungeweza kuinua mkono wako kwa uchaji? Na kusema, “Nafanya hivi, si kwa mhubiri, bali kwa Mungu. Mungu, badilisha njia yangu ya kuwazia. Nimejaribu kuwazia jinsi mambo haya yangekuwa. Nilijaribu kutoa hoja vile majirani zangu wangesema ikiwa ningezaliwa mara ya pili, kama Mungu alipata kunibariki kwa namna ambayo ningepaza sauti, kama Mungu angepata kunibariki kwa namna ambayo ningekuwa na tukio ambalo lingenifanya nilie, na ningelazimika kuwaacha wenzangu. Nimejaribu kutoa hoja zote, Mungu. Lakini, leo, sitahoji tena. Sasa hivi ninakwinulia Wewe mkono wangu, Mungu, na kusema huu ndio ushuhuda wangu. Kama utaniondolea hoja, na kuijalia nafsi yangu ichukue mahali pake kuliadini Neno Lako bila kutoa hoja, nitaamini ni sauti ya

hakika niliycopewa.” Waweza kuinua mkono wako? Mtu yeyote humu jengoni, popote ulipo. Mungu akubariki, wewe, wewe, na wewe, na wewe, na wewe. Takriban asilimia themanini na tano ya jengo hili.

²³³ Ati hoja? “Tupa chini hoja.” Zitupe chini. Mungu hataki uwe na hoja. Hoja sikuzote hujaribu kutafuta njia ya kutokea. Imani haina hoja. Imani huamini tu. Nia yako, kinachokufanya utoe hoja. Ni mwongo. Kigundua uongo kinathibitisha hilo. Biblia ya Mungu, kwanza, inalithibitisha hilo. Lakini nafsi yako haiwezi kufa, ndugu, dada. Uwezo wako wa kuhoji utakuacha wakati mauti yatakapokupiga, lakini nafsi yako itakuwa pamoja nawe katika Umilele. Hivi hutaliadini Neno la Mungu leo na kumkubali?

²³⁴ Katika maombi mafupi, mtu mwingine ungeinua mkono wako? Useme, “Nikumbuke sasa, Ndugu Branham, unapoomba. Nataka kutupilia mbali hoja.” Mungu akubariki, msichana mdogo. Yupo mwingine. Mungu akubariki, ndugu, nakuona. Mungu akubariki, ndugu, nakuona. Mungu akubariki, ndugu. Wewe, naam, dada. Mtu mwingine? Mtu mwingine inua mkono wako, upesi sana. Useme, “Kumbuka...” Mungu akubariki, ndugu mpendwa. Mungu akubariki, ndugu. Tupilia mbali hoja. Mungu akubariki, dada, ninauona mkono wako. Mungu akubariki, dada, ninauona mkono wako. Usitoe hoja tena. Amini tu. Mungu akubariki, dada.

²³⁵ Mtu mwingine, kabla tu hatujaomba sasa? Nitaomba na kumwomba Mungu kwamba atakusaidia. Anauona mkono wako. Mungu akubariki, kijana mwanamume, nauona mkono wako. Mtu mwingine? Mungu akubariki, ndugu, ninauona mkono wako.

²³⁶ Loo, baraka za kuamini! Baraka za kutojaribu kulielewa. Baraka za kutulia tu juu ya Neno la Mungu, na kusema, “Ni kweli,” na kuendelea. Ni Uzima. Ni Uzima. Ni maisha halisi.

²³⁷ Maskini mama mkwe wangu mkongwe mpendwa, anayeketi nyuma hapa, nilipokuwa nikimwelezea jana kuhusu jambo hilo. Alisema, “Billy, nilikuwa na saa ya ukutani, ambayo nisingeweza kuifanya ifanye kazi.” Kasema, “Kamwe nisingeweza kukaa bila hiyo saa. Sikuwa na pesa za kujinunulia nyingine.” Hivyo akasema, “Nilipiga magoti na kusema, ‘Mungu, nifanyie saa hiyo ifanye kazi, sivyo?’” Akasema alitazama juu, nayo ikaanza kufanya kazi, ikaendelea tu kikamilifu.

²³⁸ Friji yake, alisema, siku chache baadaye, isingeweza kuga-...iliendelea kuyeyusha barafu; mahali padogo tu ambapo ingeshikilia barafu. Alifanya kila alichoweza kufanya, kuizuia isiyeyushe barafu, au kuizuia isiyeyushe barafu, kwa sababu hangeweza kuweka siagi yake na kadhalika ndani yake. Maskini huyo mzee, yeye ni mjane.

²³⁹ Mumewe yuko Utukufuni. Huyu ni baba mkwe wangu. Alitoa ushuhuda wake wa mwisho, hapa mkono wangu wa kushoto, kabla hajaenda Nyumbani.

²⁴⁰ Akapiga magoti, alijua kwamba hakuwa na pesa za kununua friji nyingine. Akasema, “Mungu, utanirehemu tena? Unanijua mimi. Jalia friji yangu ianze kugandisha tena, sivyo?” Akasema alisimama akaenda na kuangalia ndani ya friji yake, nayo ilikuwa imegandisha kote.

²⁴¹ Kuwa rahisi. Omba tu. Usijaribu kulielewa. Usijaribu kulisoma. Amini tu. Usiliwazie kiakili. Liamini tu kwa nafsi yako.

²⁴² Baba yetu wa Mbinguni, wengi waliinua mikono yao asubuhi ya leo. Wanataka maombi. Ninaomba, Mungu, kwamba huu utakuwa ni mguso wa mwisho, leo; hawatatoa hoja tena; watakwenda, wakiamini. Tujalie, Bwana. Ni sauti inayojulikana. Ni sauti ya Injili, mwaka mtukufu wa yubile. Wakati wa ukombozi umefika.

²⁴³ Je, si Wewe, tafadhali, Baba, utamchukua kila mmoja wao katika uangalizi Wako wa upendo? Na uwape maziwa ya akili ya Injili yasiyoghoshiwa sasa. Na kama tayari wamekunywa hayo, jalia wapokee chakula kigumu sasa, na wawe Wakristo kamili; kamwe wasipige domo tena na ulimwengu, na kujifurahisha ulimwenguni; bali wawe wanaume na wanawake halisi, wakiamini sauti dhahiri, ya kwamba Injili ni ya kweli, haidhuru ni nani asemaye si ya kweli. Biblia, kila Neno, ni kweli. “Watu hufundisha Mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.” Lakini Neno la Mungu halitashindwa kamwe. Jalia wakiamini Hilo, leo.

²⁴⁴ Na wale ambao hawakuinua mikono yao, walioshawishika kweli, lakini hawakuinua mikono yao, tunawaomba, pia, Bwana, ya kwamba Wewe utawarehemu. Baraka hizi tunaomba, Baba, kwa sababu siku moja tunakuja kwenye Hukumu. Na Ujumbe wa asubuhi ya leo utaonyeshwa dhahiri kwenye Siku hiyo. Halafu jalia nafsi zao zisiwasumbue, zikisema, “Ulipaswa kufanya *hivi*.” Lakini na iwe ni amani bondeni watakapopitia huko. Kwa kuwa katika Jina la Yesu tunaomba.

... wa Miaka, uliipasuliwa kwa ajili yangu,
Nijalie nijifiche Kwako;
Jalia hayo maji na Damu,
Yaliyobubujika kutoka kwa ubavu Wako
uliojeruhiwa
Yawe tiba maradufu ya dhambi,
Yaniokoe na hasira na kunitakasa.

²⁴⁵ Mungu mpendwa, kama kukiwako katikati ya watu, siku hii, mateso yoyote, magonjwa yoyote, chochote kibaya na utu wao wa kimwili; tunaomba, Baba, kwa kuwa Roho Mtakatifu yuko hapa, akipiga makelele tu ya baraka, akizisafisha nafsi zetu na

udhalimu wote, kwa Damu ya Bwana Yesu, Mwana wa Mungu. Jalia, Yeye, leo, kwa Roho Wake mkuu wa kushawishi, sifa Zake kuu za uponyaji, jalia kila nafsi iliyo safi itazame kule Kalvari na kusema, “Huko alijeruhiwa kwa makosa yangu, na kwa kupigwa Kwake sisi tuliponywa.” Tujalie, Bwana.

²⁴⁶ Sasa tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu. Ikiwa kuna yeyote wa kuombewa, kwa ajili ya ugonjwa, naomba usimame kwa miguu yako, popote ulipo. Mungu akubariki. Hiyo ni sawa, simama tu moja kwa moja. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

...chemchemi,
Bure kwa wote, kijito cha uponyaji,
Kinatiririka kutoka kwenye chemchemi ya
Kalvari.

Msalabani, msalabani,
Uwe utukufu wangu milele; (Ewe Mungu!)
...nafsi yangu iliyonyakuliwa itapata
Raha ng'ambo ya mto.

²⁴⁷ Baba Mpendwa wa Mbinguni, Wewe unawaona hawa wote waliosimama, Baba. Wamesimama, ushuhuda, ya kwamba wanakuamini Wewe, Baba.

²⁴⁸ Wewe Ambaye ungeweza kumtuma maskini yule oposamu langoni! Wewe Ambaye ungeweza kumfanya yule fahali mkubwa, hatari, aliyekuwa amesimama pale, kisha kurudi nyuma! Wewe Ambaye ungeweza kuwafanya wale mavu kuingia katika sanduku! Wewe Ambaye ungeweza kumfufua mbwa yule, maskini mbwa wangu wa kuwinda, baada ya kukokotwa kwa mwendo wa maili sitini kwa saa, umbali wa maili mbili, amelala ameshupaa, mfu. Nilimpenda maskini jamaa huyo. Maombi yalimzindua. Maombi yaliurudisha mguu na bega la yule oposamu mahali pake, maskini mama huyo, yakamrudisha msituni, akishangilia! Mkono wa Mungu aliye hai!

²⁴⁹ Wakristo hawa wamewekeana mikono, Bwana. Nami nimeweka mikono yangu juu ya ndugu huyu, kama kutoa eneo la mawasiliano kwa kila mtu jengoni. Sisi ni waaminio, Bwana. Tunaamini mambo haya. Tunakupenda.

²⁵⁰ Hakuna sauti isiyojulikana. Tumekuona ukiwaponya wagonjwa, ukiwafufua wafu, ukiwatoa pepo wachafu, ukiondoa kansa, ukiwafanya viwete kutembea, okoa nafsi, mtakase mwaminio, mjaze Roho Mtakatifu, wape Uzima usiopatikana na mauti; wasikie wakifa, wakisifu, wakishuhudia, wakimtukuza Mungu, wakiamini Wewe unakuja tena.

²⁵¹ Tunahitaji usaidizi, Bwana. Jalia, Bwana, kwamba kila kitu kinachoombwa kitatendeka. Nafsi zitaokolewa, juu ya mambo yote; waliorudi nyuma kurejeshwa. Nasi tunaomba ya kwamba miili iliyo migonjwa itaponywa sasa hivi. Ninatuma maombi haya ya imani katika Jina la Yesu Kristo, kwa ajili ya uponyaji

wa wagonjwa, wokovu wa nafsi, kuwarejesha wale walio nje, kwa Jina la Yesu.

Imani yangu inakutazamia Wewe,
Na tusimame!

Ewe Mwana-kondoo wa Kalvari,
Mwokozi wa Kiungu;
Nisikie sasa niombapo,
Ondoalea mbali hatia yangu yote,
Wala usiniache nipotee
Kutoka Kwako kwenda kando.

²⁵² Sasa ninyi mnaoweza, inueni mikono yenu, tunapouimba huu:

Ninapopitia kwenye mzingile wenye giza,
Na huzuni zinasambaa kunizunguka,
Loo, kuwa Kiongozi wangu Wewe;
Agiza giza ligeuke kuwa mchana,
Yapanguse machozi ya huzuni,
Wala usiniache nikatangatange
Kutoka Kwako kwenda kando. 

55-0731 Sauti Isiyojulikana
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org